# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA SHERIA, UTAWALA BORA NA IDARA MAALUM YA BARAZA LA WAWAKILISHI – KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar, 1984 na Kanuni ya 106(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la 2016 na kuainishwa majukumu yake chini ya Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo kama ifuatavyo:-

i) Kufuatili utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.
iii) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
iv) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa bajeti wa wizara zifuatazo:

- Wizara ya Nchi (OR) Katiba,Sheria,Utumishi wa Umma na Utawala Bora
- Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita

i) Unguja wiki mbili tarehe 29 Ogasti 2016 hadi tarehe 9 Septemba, 2016.
ii) Pemba wiki moja tarehe 31 Oktoba 2016 hadi tarehe 4 Novemba, 2016. na Unguja wiki moja kuanzia tarehe 7 hadi tarehe 11 Novemba, 2016.
iii) Unguja wiki moja 16 Januari 2016 hadi tarehe 20 Januari 2016 na Pemba 23Januari 2016 hadi tarehe 27 Januari 2016.

## MUUNDO WA KAMATI

Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | - | Makamo M/kiti |
| 3. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammed Said Mohammed | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Ali Alawy Ali | - | Katibu |

**HADIDU REJEA**

Kamati ilifanya kazi zake kwa kutumia Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2016, Hotuba za bajeti za Taasisi za Wizara za Serikali za mwaka 2016/2017 pamoja na Taarifa za Taasisi husika za Serikali.

## SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA NCHI (OR) KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA.

Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaundwa na idara zifuatazo:

1. IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI
2. IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI
3. IDARA YA MIUNDO YA TAASISI ,UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI
4. IDARA YA MIPANGO YA RASILIMALI WATU
5. IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA
6. IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (E-GOVERNMENT)
7. IDARA YA UTAWALA BORA
8. OFISI YA AFISA MDHAMIN PEMBA

Aidha, Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:-

1. OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI
2. OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA SERIKALI
3. MAHKAMA
4. TUME YA UTUMISHI YA MAHKAMA
5. OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA
6. OFISI YA MUFTI
7. TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA
8. KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA
9. TUME YA UTUMISHI SERIKALINI
10. TUME YA UTUMISHI WA MAHKAMA

11. KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA
12. OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI
13. TUME YA KUREKEBISHA SHERIA
14. MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kiungo kikubwa katika Wizara hii na taasisi nyengine za Serikali ambapo Kamati ilipatiwa maelezo juu ya majukumu ya Idara hii na jinsi inavyosimamia na kuratibu shughuli zote za Wizara.

**IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA:**

Idara ya nyaraka na kumbumbu za taifa ni moja kati ya idara muhimu sana yenye jukumu la kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka zote za Serikali na kuhakikisha kuwa zinahifadhiwa katika hali ya usalama kwa matumizi ya Taifa.

**CHANGAMOTO ZA IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA**

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika ofisi yake iliyopo kilimani na kubaini changamoto zifuatazo:-

1. Wana changamoto ya usafiri ambapo hadi sasa wana gari moja tu na kutokana na uhaba huo wameona wanunue vespa moja kuweza kusaidia lakini bado tatizo la usafiri lipo katika utekelezaji wa kazi zao.
2. Pia wana tatizo la upungufu wa wafanyakazi.
3. Kamati imeelezwa kuwepo kwa tatizo kwa Wizara za serikali kuwa na mrundikano wa nyaraka na faili ambazo zinazagaa na baadae kupotea faili ambazo ni muhimu bila kuchukuliwa hatua zinazotakiwa za uhifadhi.
4. Kamati imeelezwa kuwa wafanyakazi wa chumba cha kuhifadhia nyaraka (strong room) wanakabiliwa na tatizo la afya kwa sababu ya kutumia kemikali.
5. Kamati pia imejuilishwa kuwa kuna ukosefu wa (incinirator)

Pia kamati imegundua baadhi ya changamoto katika maeneo kama ifuatavyo:-

**Changamoto Zinazoikabili Sehemu ya Strong Room**

1. Ukosefu wa vipoza hewa zaidi ya 4 vyenye uwezo wa tani 2 au zaidi na fani 2.
2. Ukosefu wa makabati ya chuma ya kuhifadhia ramani na plan.
3. Uchakavu wa chumba husika sababu kuna sehemu ina unyevu unyevu wa kukaa kwa maji ndani ya dari.
4. Ukosefu wa free acidic box kwa kuhifadhia kumbukumbu zinazohitaji kuhamishiwa katika Strong room.
5. Upungufu wa vifaa vya kufanyia kazi za kila siku katika chumba hiki ikiwemo kitoroli cha kubebea majalada, transparent envelops, brown papers n.k.
6. Nyaraka nyingi kuchakaa na kupoteza haiba yake kwa kukosekana kwa vifaa vya kuhuisha na wataalamu wenye utaalamu unaohitajika kwa kazi hiyo.

7. Mazingira yasiyoridhisha ya kufanyia kazi hasa ukitilia maanani umuhimu wa afya za wafanyakazi ingawaje wanalipwa 125,000/= za mazingira magumu ya kazi, pamoja na kukosekana kwa upimaji wa afya za wanyakazi.
8. Ukosefu wa mafunzo kwa watendaji.

**Changamoto zaUsimamizi wa Kumbukumbu (Records Management Unit).**

1. Ukosefu wa Usafiri kwa kazi za ukaguzi.
2. Kutotengewa bajeti katika kazi za ukaguzi.
3. Kutokuwepo kwa uelewa wa umuhimu wa utunzaji na uhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika taasisi nyingi za serikali na mashirika yake.
4. Wakuu wa taasisi na mashirika ya serikali hawatilii maanani umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka dhidi ya juhudi na bidii zinazofanywa na watendaji wa kitengo hiki.
5. Mrundikano na upotevu mkubwa wa kumbukumbu na nyaraka katika taasisi na mashirika ya serikali kutokana na ukosefu wa kituo cha uhifadhi wa kumbukumbu zilizofungwa (Semi Current Records)
6. Taaluma ndogo kwa watendaji wengi wa masjala na wasimamizi wa kumbukumbu

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri kutumiwa vifungu vya fedha za kuhifadhia nyaraka viliopo Serikalini viwe vikiingizwa idara ya nyaraka ili waweze kuvitumia katika shughuli zao za kuhifadhi nyaraka na ukaguzi wa nyaraka hizo badala ya kutegemewa bajeti ndogo wanayotumia hivi sasa ambayo haikidhi haja.
2. Kamati inashauri suala liliopo sasa kwa wizara za Serikali zinazotaka kuondokana na mfumo wa nyaraka (documents) na badala yake kuwa na mfumo wa digitali kuwa zisibadilike na kuondokana kabisa na mfumo wa zamani kwa kuzichoma moto nyaraka lakini badala yake wawe na mifumo yote miwili kwani mfumo wa digitali sio wa kuaminika sana.
3. Kamati inasisitiza serikali kuchukua jitihada za kuwatafutia usafiri idara ya nyaraka ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kazi ipasavyo.
4. Kamati inaagiza idara ya nyaraka kupitia wizara ya Katiba kulifanyia kazi suala zima la upimaji wa afya za wafanyakazi kila mda unapofika kutokana na utumiaji wa kemikali kali za kuhifadhia nyaraka ambazo zinaathiri afya zao.
5. Kamati inaishauri Serikali kulichukulia umuhimu suala zima la kuwepo kituo maalum cha kuhifadhia kumbukumbu ambacho kitawezesha kuzuia upotevu mkubwa wa nyaraka na kumbukumbu uliopo sasa katika Taasisi za Serikali pamoja na kupunguza msongamano wa kumbukumbu zilizofungwa katika maofisi na Taasisi za Serikali. Hali hii itasaidia kuleta ufanisi katika shughuli za usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka.
6. Pia kamati inaagiza kupatiwa mafunzo watendaji wa idara ya nyaraka hasa wanaohudumia chumba maalum cha kuhifadhia nyaraka (strong room) ili waweze kufanya kazi zao kwa utaalamu zaidi na kwenda na wakati katika suala zima la uhifadhi wa nyaraka.

7. Kamati imesikitishwa na taarifa ya ukosefu wa vitendea kazi muhumu vinavyohitajika katika kutunza na kuhifadhi kumbukumbu hizo, hivyo kamati inaiagiza wizara kuchukua jitihada za makusudi na kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana.
8. Kamati inaagiza katika kuhakikisha suala la usalama linaimarishwa katika Ofisi ya Nyaraka basi iwekwe smoking alart ambayo itatoa ishara iwapo mtu atapita na kitu kisichokua cha kawaida.
9. Kamati inaagiza nyumba iliyopo ndani ya eneo la idara ya nyaraka inunuliwe na Serikali ili kuepuka athari zinazoweza kuja kutokea za kiusalama.

**OFISI YA AFISA MDHAMIN PEMBA**

Ofisi ya Afisa Mdhamin Pemba ni kiungo muhimu katika kusimamia na kuratibu shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Kamati ilipata fursa ya kutembelea ofisi hiyo na kubaini yafuatayo:

**CHANGAMOTO ZA OFISI YA AFISA MDHAMIN PEMBA**

1. Kamati imebaini kuwa wana changamoto ya ukosefu wa ofisi na uchakavu wa jengo la ofisi wanalotumia kwa sasa ambapo inawabidi kutumia pesa nyingi kwa kufanya ukarabati.
2. Kamati pia imebaini kuwa kuna baadhi ya idara haziingiziwi fedha za matumizi moja kwa moja isipokua zinaingizwa katika kurugenzi zao kuu ziliopo Unguja kitu ambacho kinasababisha Ofisi kuu Pemba kutumia fedha zao kwa ajili ya kuendeshea wa Idara hizo.
3. Kutokuwepo kwa baadhi ya Taasisi kwa Ofisi Kuu Pemba ikiwemo:

(i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu
(ii) Tume ya Kurekebisha Sheria
(iii) Tume ya Utumishi Serikalini, na
(iv) Ofisi ya Serikali Mtandao (E- Government)

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua zinazofaa suala la kutoingizwa fedha za matumizi moja kwa moja katika baadhi ya idara za Pemba.
2. Kamati pia inaagiza kufanyiwa haraka uwepo wa Taasisi zilizokosa ofisi huko Pemba ili kuondoa changamoto zinazojitokeza kwa kukosekana ofisi hizo.
3. Suala la ukosefu wa Ofisi ya Afisa Mdhamin Pemba, Kamati inaomba kuangaliwa kwani hali ilivyo sasa inasababisha gharama zisizokua na maana kwa Serikali.
   Aidha, Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia Taasisi zinazojitegemea kama zifuatavyo:-

**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa ushauri juu ya masuala ya sheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi zake. Mbali na jukumu hilo ofisi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

1. Kamati imeelezwa kuwa kuna ukosefu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa upande wa Pemba kitu ambacho kinaipa changamoto kubwa Ofisi hii katika utekelezaji wa kazi zake.
2. Sula la kuwemo makosa katika miswada, kuchelewa kuletwa Barazani pamoja na miswada kuwa na utofauti kati ya miswada ya Kiengereza na Kiswahili. Kamati imeelezwa kuwa tatizo kubwa ni muda ambao miswada hiyo inapelekwa kutoka Taasisi au Idara inayohusika na mswada huo, kwani hupelekewa miswada muda mdogo na kutakiwa haraka kwa ajili ya kuwasilishwa Barazani.
3. Kamati imeelezwa kuwa kuna uhaba wa wafanyakazi katika vitengo mbali mbali ndani ya afisi ya Mwanasheria Mkuu.
4. Kamati imeelezwa pia katika suala la uendeshaji wa kesi za Serikali kuna changamoto katika suala zima la ushirikiano kutoka katika Taasisi za Serikali pale wanapohitajika na Ofisi ya AG kitu ambacho kinapelekea muda mwengine Serikali kushindwa kesi zake.
5. Tatizo la usafiri liliopo ni changamoto kwa ofisi ya AG.
6. Kamati imeelezwa changamoto nyengine ni kuwepo na tatizo katika mikataba ya Serikali katika suala zima la utekelezaji kwani kumekua na tabia kwa Taasisi za Serikali kupitia Serikali kuu ya kuitaka ofisi ya AG ivunje mikataba wakati ambapo mkataba husika umeshalipwa asilimia tisini (90%) ya pesa kitu ambacho huwa ni hasara kwa Serikali. Na changamoto hii husababishwa na usimamizi mbovu wa mikataba hiyo kutoka mawizarani au Taasisi mbali mbali za Serikali.

Kutokana na changamoto hizo kamati inatoa maoni na maagizo yafuatayo:

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kutokana na changamoto ya ukosefu wa ofisi kwa upande wa Pemba kamati inaiagiza wizara kulifanyia kazi suala hilo ili kuondokana na changamoto iliyopo sasa kwani kuwepo kwa ofisi kwa upande wa Pemba ni muhimu katika utekelezaji mzuri wa masuala yote yanayohusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.
2. Kamati inazitaka Taasisi za Serikali kutoa ushirikiano kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pale wanapohitajika katika masuala ya kesi zinazoikabili Serikali.
3. Kamati inaiagiza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kulichukulia umuhimu suala la kuajiri wafanyakazi ili kukidhi haja katika kutekeleza majukumu yao pamoja na kuwapatia mafunzo ili waweze kufanya kazi kitaalamu zaidi katika vitengo vyao.
4. Katika suala la uchelewaji miswada pamoja na kuletwa miswada kuwa na mapungufu mengi na yasiyo ya lazima katika Baraza, kamati inaziagiza Wizara za Serikali kuwashirikisha wanasheria wa serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tokea katika hatua za awali na sio kuwapatia wanashaeria hao mswaada husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi. hii itapelekea kuondokana na changamoto zisizokuwa za lazima ndani ya Miswada inayowasilishwa Barazani.
5. Kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi zake kuzingatia na kusimamia kwa umakini mkubwa masharti ya mikataba, hii itaisadia Serikali kuokoa fedha nyingi ambazo

zinapotea kutokana na kutokuwepo kwa wasimamizi madhubuni wa mikataba hasa katika Taasisi za Serikali, lakini pia, itaisaidia Serikali kuepusha kushitakiwa mara kwa mara kwa kuvunja mikataba hiyo.

**OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina jukumu la kukagua mahesabu ya Taasisi za Serikali na Mashirika na kutoa tarifa zake kila mwaka.
Kamati katika kazi zake ilipata fursa ya kufanya ziara kwa ofisi za Unguja na Pemba ambapo imeelezwa Kamati; mbali ya kutekeleza jukumu hilo Ofisi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO ZA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)**

1. Kamati imeelezwa kuwa changamoto kubwa inayowakabili ni ufinyu wa bajeti.
2. Upungufu wa wataalamu katika fani kama vile uhandisi ni kitu ambacho kinawalazimu waajiri wataalamu kutoka nje ya ofisi kwa ule muda wanaowahitaji katika kazi zao. Kitu ambacho ni gharama kubwa kwa Serikali.

3. Kuwepo na baadhi ya mashirika yasiyotoa ushirikiano wakati wa kazi za ukaguzi zinapofanyika, kitu ambacho huwa ni changamoto katika utekelezaji wa kazi zao.

4. Kamati pia imeelezwa kuwa kuna kilio kikubwa cha maslahi kwa wafanyakazi wa ofisi ya CAG kwani hadi sasa wanapokea mshahara wa kawaida tu na ukilinganisha na kazi zao kidogo inakua ni kikwazo kwa sababu kazi ngumu ila maslahi madogo. Lakini vile vile kutokana na kazi zao zinaweza kuwasababishia kufanya ubadhilifu wa fedha wakati wa kufanya ukaguzi kwa tamaa ya fedha na hali halisi ya maisha lakini iwapo Serikali itawatizama kimaslahi basi itasaidia kuwaepusha na changamoto hizo.

5. Kwa upande wa Ofisi ya CAG Pemba kamati imejuilishwa kuwa hadi sasa wana changamoto ya ukosefu wa baadhi ya wataalamu katika baadhi ya fani ambapo inapotokea kazi inabidi watoke watu ofisi kuu Unguja kuja kufanya kazi ambayo wangelikuwepo wataalamu basi wangeifanya.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

**1.** Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala la bajeti kwani ufinyu wa bajeti katika ofisi ya CAG kunaweza kukwamisha shughuli zao za kazi ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya Nchi yetu katika masuala mazima ya ukaguzi wa fedha za Serikali.
**2.** Kamati pia inaishauri Serikali katika kuhakikisha inafatilia vyema matumizi ya fedha zake, ikawapatia wafanyakazi wenye taaluma mbali mbali ambazo watahisi zinaweza kuwasaidia kwa upande wa Unguja na Pemba.
**3.** Kamati inasikitishwa na kitendo cha baadhi ya Mashirika kutotoa ushirikiano wakati wa kazi za ukaguzi zinapofanyika kitu ambacho kinakwamisha utekelezaji mzuri wa kazi.

Kamati kupitia changamoto hii inamuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuwachukulia hatua wale wote wasiotoa ushirikiano katika kutekeleza wa kazi za ukaguzi.

**4.** Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala la maslahi kwa wafanyakazi wa CAG ili kuzuia changamoto ya ubadhirifu katika ukaguzi.

**MAHKAMA**

Mahkama ni moja kati ya mhimili muhimu katika nchi ambao una wajibu wa kuhakikisha haki za raia wake zinapatikana kwa mujibu wa sheria za nchi.

Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilifanya ziara kwa baadhi ya Mahkama za Unguja na Pemba na kugundua kuwa hukumu inayotolewa kwa vitendo vya udhalilishaji bado ndogo, uchakavu wa mahkama, ushirikiano mdogo kati ya mahkama,muendesha mashtaka na polisi na wananchi (mashahidi).

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha mahkama za watoto kwa Unguja na Pemba ambazo zitasaidia katika uendeshaji wa kesi zote zinazohusu watoto na kurahisisha upatikanaji wa haki za mtoto.

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara kwa upande wa Unguja Mahkama Kuu Vuga, Mahkama ya Mwanakwerekwe, Mahkama ya Mfenesini na kwa upande wa Pemba Mahkama ya Cheke Chake, Wete na Mkoani na kubaini changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAHKAMA**

1. Kamati katika ziara yake kwa upande wa Mahkama ya Vuga imeelezwa kuwepo kwa changamoto ya jengo bado dogo na halikidhi haja. Vile vile wameiarifu Kamati kuwa wamepewa kiwanja Tunguu lakini ni kidogo kwa ujenzi wa Mahkama Kuu. Hata hivyo, wameeleza kuwa katika mazingira kote ulimwenguni Mahkama Kuu zinakaa Mjini na sio nje ya miji.
2. Kuna ongezeko la kesi za ubakaji na udhalilishaji na jamii kutokua na uelewa wa kutosha juu ya kesi hizo.
3. Kamati imejuilishwa kuwa suala la kesi za madawa ya kulevya kuwa halipo katika ngazi ya mahkama kwani wao hupokea taarifa kutoka kwa Wakala wa Mkemia Mkuu na kuifanyia kazi kama ilivyoelezwa, kamati imeona ni changamoto kwani kumekua na malalamiko mengi ambayo yanaihusisha ofisi ya mkemia mkuu wa serikali katika kesi za madawa ya kulevya.
4. Suala la mrundikano wa kesi lipo lakini wameiambia kamati suala hili zaidi linatokana na mashahidi kutofika kutoa ushahidi na kupelekea kesi kukaa mda mrefu bila kutolewa hukumu.
5. Pia kamati imeelezwa kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa Majaji kwa Unguja na Pemba kwani hadi sasa wapo sita (6) ambao hawatoshelezi. Pia imeelezwa kuwa kumefanyika jitihada za kukaa na Mhe Rais wa Zanzibar juu ya suala hili na wakapatiwa ridhaa ya kuongeza Majaji lakini changamoto iliyojitokeza ni ukosefu wa pahala pa kuwaweka kwa sababu waliokuwepo sasa wanachangia ofisi.

6. Vile vile, wameiarifu Kamati kuwa suala la ukosefu wa Majaji kwa upande wa Pemba kweli lipo lakini kikwazo kikubwa kwa sasa ni vigumu kumuweka Jaji wa kudumu Pemba, kwa vile kesi za kusikiliza ni kidogo sana lakini pia kuna ukosefu wa nyumba za makaazi kwa Majaji.
7. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa changamoto ya vitendea kazi ambapo kwa kiasi kikubwa inachangia kurundikana na kuchelewa kwa kesi.
8. Kukosekana kwa wakemia na mashine za kupimia vielelezo nayo imeelezwa kuwa ni changamoto inayopelekea kurundikana kwa kesi.
9. Katika suala zima la kuwepo kwa wingi wa kesi za trafiki, Kamati imeelezwa ni vyema ikaangaliwa sheria katika masuala ya fine kama ni ndogo au zinahitaji kufanyiwa marekebisho.
10. Kuna changamoto katika bajeti; Mahkama wameieleza Kamati angalau basi wangepatiwa mfuko wao na kuachana na tabia ya kutegemea fungu kutoka wizarani kitu ambacho hupelekea kuzorota kwa kazi za Mahkama.
11. Kamati vile vile imejuilishwa kuwa suala la uingizaji na utumiaji wa madawa ya kulevya ni changamoto kubwa iliyopo na limekua na utaratibu wa kumalizwa kesi zake kwa rushwa lakini pia na upande mwengine polisi nao huchangia kuharibu kesi hizi.

***Kamati katika ziara yake kwa Mahkama ya Mwanakwerekwe imebaini changamoto zifuatazo:-***

**1.** Kamati imetembelea jengo na kuona ni dogo sana halina nafasi, bovu na chakavu linahitaji matengenezo makubwa na ya haraka ambapo kamati imeona chumba kimoja cha ofisi kinatumiwa na mahakimu wawili na ofisi za mahkama zinatumiwa na watu zaidi ya kumi na chumba cha mahabusu kidogo sana kinahatarisha afya zao.
2. Mahkama pia ina ukosefu wa vitendea kazi pamoja na makabati ya kuhifadhia majalada hali amabayo kamati haikuridhika nayo kwani hayapo katika sehemu salama.
3. Kamati imejuilishwa kuwa pesa zote zinazohusu miradi ya mahkama zinakwenda moja kwa moja wizarani kitu ambacho kinawakwaza utekelezaji wa miradi hiyo tofauti na awali ambapo zilikua zikiingizwa katika bajeti ya Mahkama.
4. Pia Kamati imejuilishwa kuwa sheria ya adhabu namba 6 ya 2004 ina matatizo katika uendeshaji wa kesi.
**5.** Kamati imeelezwa kuwa kuna kiwanja maeneo ya Mwanakwerekwe ambacho ni cha ujenzi wa mahkama mpya lakini changamoto iliyopo ni fedha za ujenzi wa Mahkama hiyo.

***Kamati pia ilifanya ziara kwa Mahkama ya Mfenesini na imebaini changamoto zifuatazo:-***

1. Pia kamati ilifanya ziara katika Mahkama ya Mfenesini na kuona hali ya jengo likiwa halifai kabisa, halina nafasi, lakini hadi leo bado wana choo kimoja ambacho wanatumia Mahakimu, Makarani,mahabusu na wananchi wanaokuja katika kufatilia kesi zao.
2. Kamati pia imeelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti kwa mahkama inapelekea kukosekana hata pesa za kuwalipa mashahidi wanaotakiwa kuja Mahkamani kutoa ushahidi kitu ambacho kinapelekea kesi nyingi kuzorota na hatimae kukosekana kwa ushahidi.

3. Katika ziara hiyo kamati ilijionea jengo la ukumbi wa kusikilizia kesi ambalo limejengwa mda mrefu na halijawahi kutumika, na kwa sasa halifai kwani lina nyufa kubwa ambazo zinahatarisha usalama wa maisha ya watu.
4. Kamati imebaini kuna uhaba na uchakavu wa vitendea kazi kwa shughuli za mahkama.
5.

***Kamati pia ilifanya ziara kwa Mahkama ya Chake Chake na imebaini changamoto zifuatazo:-***

1. Kamati imejionea kuwa kuna uchakavu wa majengo ya mahkama hasa kwa mahkama ya Wete na Mkoani ambapo ilifanya ziara lakini pia kamati imejuilishwa kuwa baadhi ya majengo ya mahkama ni machakavu na yanahitaji matengenezo makubwa kama vile, Mahkama ya Wilaya Konde na Mahkama ya Kengeja.
2. Vile vile kuna changamoto ya upungufu wa watumishi katika kada ya Sheria, Manunuzi, Mtunza ghala, Matarishi, walinzi na watu wa hesabu.
3. Pia kamati imeelezwa kuwepo na uhaba wa gari pamoja na nyumba za kuishi Majaji na Mahakimu kitu ambacho kinapelekea hasara kubwa kwa Serikali kwani inawalazimu kukodi.
4. Ufinyu wa bajeti ambao unapelekea Mahkama kutofikia malengo yake yaliyojipangia pamoja na kushindikana kusomesha wafanyakazi wake.
5. Kamati pia imeelezwa kuwa katika uendeshaji wa kesi kuna tatizo la mashahidi kutofika kutoa ushahidi kitu ambacho kinakwaza shughuli za mahkama lakini pia kinapelekea kesi nyingi kufa kutokana na kukosekana kwa mashahidi

***Kamati pia ilifanya ziara kwa Mahkama ya Wete na Mkoani imebaini changamoto zifuatazo:-***

1. Kwa upande wa Mahkama ya Wete nayo hairidhishi katika mzingira ya kazi kwani jengo lake ni bovu na halina nafasi ya kutosha.
2. Hawana vitendea kazi kama makabati ya kuhifadhia majalada, wana kompyuta moja lakini hata meza na viti havifai.
3. Mahkama ya Mkoani jengo limefanyiwa matengenezo kupitia mradi wa ZUSP lakini matengenezo hayo yamefanyika kwa upande wa nje tu wa mahkama hali ambayo haileti picha nzuri kwa upande wa ndani.
4. Mahkama hii nayo ina changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi ikiwemo fotokopi mashine ambapo kamati imeona ni changamoto kutolewa nje kazi za Serikali.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaagiza kufanyiwa kazi suala zima la udhalilishaji kwani limekua ni changamoto kubwa inayoikabili jamii na hata kukosekana imani kwa chombo cha mahkama na jamii.
2. Kamati imebaini kuwepo na idadi kubwa kwa rumande kuliko wanafunzi kitu ambacho kimekua kikiipatia hasara serikali kila siku kwani kuwepo kwao kunailazimu serikali kuwahudumia. Hivyo, kamati inaziagiza mahkama izifanyie haraka kesi hasa za mazao na mifugo kwa kuzitolea maamuzi kwa lengo la kupunguza mrundikano wa rumande kama ilivyo sasa ivi.

3. Kamati inaagiza kufanyiwa kazi suala la vitendea kazi kwa Mahkama zote Unguja na Pemba.
4. Kamati inashauri kuanza mara moja ukarabati wa jengo la Mahkama ya Mwanakwerekwe kwa fedha wazizotengewa kwani liko katika hali mbaya. Kamati inaona ni busara kwa vile kiwanja kipo basi wafanye jitihada za kuanza ujenzi wa mahkama hiyo ambayo itakua na nafasi zaidi na itaondoa tatizo ukosefu wa nafasi.
5. Kamati inaigiza wizara kufanya jitihada za makusudi kujenga Mahkama ya Mfenesini, Wete, Konde na Kengeja.
6. Kamati inaishauri wizara kufanya jitihada za kukarabati jengo la Mahkama ya Mkoani kwa upande wa ndani ambao haukukarabatiwa na mradi wa ZUSP ili kuleta haiba na kuwa na mazingira mazuri ya kazi kwani yaliyopo sasa hayaridhishi.
7. Kamati inaishauri Mahkama kuandaa program maalum ya kutoa elimu kwa jamii juu ya sheria ya ushahidi katika masuala ya kesi za udhalilishaji ili jamii kuwa na muamko juu ya ushahidi upi unaotakiwa kisheria na hatua gani wafanye pindi linapotokea tatizo lakini pia waweze kushajihishwa juu ya umuhimu wa kutoa ushahidi.
8. Kamati imeshauri katika masuala ya kesi na utoaji wa ushahidi ni vyema ikawepo sharia ya **"Protection act"** ambayo itawalinda watoaji ushahidi kama ilivyo kwa wenzetu Kenya.
9. Kamati imeona ni busara kuwepo na kifungu maalum cha kuwalipa mashahidi angalau pesa ya nauli ili kuwashajihisha katika umuhimu wa kutoa ushahidi unaotakiwa mahkamani.
10. Kamati inaliona suala la nyumba za kukaa Majaji litizamwe kwani muhimu hasa kwa upande Pemba.
11. Pia kamati inashauri kurejeshwa utaratibu wa Mahkama kuwa na fungu lao na kuachana na kutegemea fungu kutoka wizarani ili kupunguza changamoto zinazojitokeza kutokana na utaratibu huo.
12. Kamati inaishauri Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kufatilia na kufanya uadilifu wa hali ya juu katika kesi zinazohusu madawa ya kulevya ili kuisaidia Serikali katika vita dhidi ya madawa ya kulevya.
13. Kamati inaagiza kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho sheria ya adhabu namba 6 ya mwaka 2004 ili kuondoa changamoto zilizopo sasa katika utekelezaji wa sheria hiyo.

**OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni moja kati ya Taasisi muhimu katika kusimamia masuala yote yanayohusu kesi za jinai. Kamati lipata fursa ya kufanya ziara kwa ofisi zake kwa upande wa Unguja na Pemba na kubaini yafuatayo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA UNGUJA.**

1. Uhaba wa bajeti hali amabayo inakwaza katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.
2. Uhaba wa waendesha mashtaka kwa upande wa Unguja na Pemba kitu ambacho kinawakwaza utekelezaji wa kazi zao.
3. Kamati imejuilishwa kuwepo na changamoto ya kutokamilika kwa ushahidi katika majalada yanayowasilishwa na polisi kitu ambacho kinapelekea jamii kutokua na imani

na ofisi ya DPP na kuona ofisi inawanyima haki lakini ukweli ni kuwa majada hayo hukosa ushahidi toka yanapokuja kutoka kwa polisi.

4. Kamati imeelezwa kuwepo na changamoto ya usalama katika utekelezaji wa kazi zao ambapo hupokea vitisho mbali mbali kutoka kwa washtakiwa wakati wa kuendesha kesi.
5. Katika suala zima la kesi za madawa ya kulevya imejuilishwa kamati kuwa ni tatizo na tatizo hilo hujitokeza zaidi katika utunzaji wa vielelezo, pamoja na kukosekana kwa uaminifu na uadilifu kwa watendaji wenyewe.
6. Kesi za udhalilishaji kamati imejuilishwa kuwa nayo ni changamoto inayoiumiza jamii na wahusika wa kesi hizo ni watu wa karibu wa muathirika. Lakini pia kuna tabia ya wanajamii kumalizana wenyewe kwa wenyewe,kukataa kutoa ushahidi katika kesi hizo pamoja na kupeleka maombi ya kufutwa kwa kesi.

***Kamati kwa upande wa Ofisi ya DPP Pemba imebaini yafuatayo:-***

1. Kwa upande wa Ofisi ya DPP Pemba kamati imejuilishwa kuwa kuna changamoto kubwa ya jengo la ofisi ambapo hadi sasa wanakaa jengo la kukodi na pia halitoshelezi kwani lina ufinyu wa nafasi.
2. Pia kamati imejuilishwa kuwa Ofisi ya DPP Pemba ina uhaba wa gari ambapo ina gari moja ambayo inatumika kwa kazi zote za mashtaka wakati kazi hizo zinafanyika katika Mahkama zote za Pemba na inakua ni changamoto kubwa katika kutekeleza majukumu yao.
3. Vile vile kamati imejuilishwa kuwa idadi ya waendesha mashtaka ni ndogo na haitoshelezi hadi sasa lakini pia wana uhaba wa wafanyakazi kama vile wachapaji, mtunza ghala, mkutubi, afisa manunuzi na walinzi.
4. Kuna changamoto ambayo imejuilishwa kamati ya ukosefu wa ushirikiano wa wasimamizi wengine wa haki za jinai ikiwemo jeshi la polisi katika dhana ya upelelezi kwanza na Mahkama kuchelewesha hukumu na hati za mwenendo wa kesi kwa ajili ya rufaa.
5. Kamati imeelezwa kuwa kesi nyingi zinazopelekwa kwao ni kesi za walimu wamadrasa dhidi ya watoto wadogo na kesi za watoto chini ya miaka 18 yaani miaka 15,16,17 na 18 ambapo wahusika wanaona kesi hizi za chini ya miaka 18 sio kosa kwa vile wamependana wenyewe na kusahau kama sheria inasema ni kesi za ubakaji. Ambapo hali hii husababisha ongezeko kubwa la makosa haya na kuongezeka kwa mimba za umri mdogo siku hadi siku.
6. Kamati imeelezwa kuwa kesi za madawa ya kulevya ambazo hubainika kwa kupimwa mkojo zipo Pemba lakini utaratibu zinatakiwa kesi hizi ziende kwa Mkemia Mkuu kwa ajili ya uchunguzi na Ofisi ya Mkemia Mkuu kwa upande wa Pemba ina mfanyakazi mmoja ambapo huwa changamoto katika ufanikishaji wa kesi hizi.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri kuwepo na mashirikiano kati ya jeshi la polisi na DPP ili lengo la uendeshaji na utoaji wa haki kufikiwa na pia kuwawezesha wananchi kuwa na Imani na Serikali yao katika masuala ya upatikanaji wa haki.
2. Kamati inaagiza kufanyiwa marekebisho ya sheria namba 4 ya mwaka 2005 ya kuwalinda wari na wajane ambayo ina tatizo kwani haiwezi kumshataki mtu ambae

atampa mimba mtoto chini ya umri wa miaka 18 na kusababisha upande mmoja kukosa haki katika kesi hizo.

3. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua za haraka za kuajiri waendesha mashtaka na wafanyakazi wengine hasa kwa upande wa Pemba ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.
4. Pia kamati inaiagiza wizara kulifanyia kazi suala la usafiri kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba ili waweze kutekeleza kazi zao ipasavyo.
5. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua wale wote wanaofumbia macho vitendo vya udhalilishaji kwa kumalizana wenyewe kwa wenyewe, wanaokataa kutoa ushahidi na wanaopeleka maombi ya kufutwa kwa kesi za udhalilishaji kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwani hali hii inachochea kuongezeka vitendo vya udhalilishaji na kuwapa mwanya wafanyaji wa vitendo hivyo.
6. Kamati inaagiza kuwa suala la ushirikiano katika masuala ya haki za jinai liwe ni la lazima kwa wale wote wanaohusika ili uendeshaji wa kesi na upatikanaji wa haki uwepo kwa wakati.
7. Kamati inaiagiza wizara kupitia Wizara ya Afya kufanya utaratibu wa kuongeza wafanyakazi kwa ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu Pemba ili kesi zote zinazohusu madawa ya kulevya ziweze kuendelea kiutaratibu na kuondokana na malalamiko yaliyopo sasa kwa vyombo vya upatikanaji wa haki.

**OFISI YA MUFTI**

Ofisi ya Mufti ina jukumu la usimamizi na uratibu wa masuala mbali mbali ya dini ya kiislam yanayohusu utatuzi wa migogoro katika familia, masuala ya ndoa na talaka, fat - wa kwa misingi ya kiislam, usajili wa vyuo vya Qur-an na misikiti, ziara za kutembelea miskiti na vyuo vya Qur-an, kukutana na viongozi mbalimbali wa kijamii pamoja na taasisi za kiislam.

Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Mufti kwa upande wa Unguja na Pemba na kugundua yafuatayo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MUFTI**

1. Bajeti ndogo na haikidhi haja.
2. Vile vile ofisi ya Mufti haina voti yake wenyewe hali ambayo inaleta shida katika utekelezaji wa majukumu yao.
3. Kamati imeelezewa kuwa masuala ya vitendo vya jinsia moja yapo na yameenea sana na wafanyaji wa vitendo hivyo ni watu wenye pesa.
4. Pia wameelezea suluhu juu ya masuala haya ya vitendo vya jinsia moja ni kutoa elimu kwa jamii lakini wanashindwa kwa vile bajeti ndogo sana.
5. Kamati imeelezwa kuna uhaba wa wafanyakazi hasa katika kitengo cha Fat-wa kwa uapande wa Unguja na Pemba.
6. Kamati imeelezwa kuwa suala la kuharibiwa watoto na walimu wa madrasa lipo kweli na kwa sasa wana utaratibu wa kutoa elimu na mpango wa sasa wanataka wawe na utaratibu wa kutoa vyeti maalum kwa walimu wote wa madrasa.
7. Kuhusiana na suala zima la baadhi ya maimamu kujihusisha na siasa ofisi ya Mufti imeeleza kuwa suala lipo na wanapomgundua Imamu anahubiri siasa basi wanamchukulia hatua.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati imeshauri ofisi ya Mufti kuwa na mashirikiano na ofisis ya DPP katika kesi za walimu wa madrasa ili kuweza kujua na kupata taarifa juu ya kesi hizo.
2. Kamati inaishauri suala la vitendo vya jinsia moja ofisi ya Mufti itoe barua kwa Maimamu wote ili watoe elimu ndani ya miskiti kwa lengo la kuisaidia jamii juu ya janga hili.
3. Kamati inaiagiza wizara ya Katiba kulichukulia hatua suala la Ofisi ya Mufti kupatiwa voti yake na kuongezewa bajeti kwa mwaka ujao ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.
4. Kamati inaagiza kupatiwa wafanyakazi Ofisi ya Mufti ili waweze kutekeleza kazi zao ipasavyo.
5. Kamati inashauri kuchukuliwa hatua na kulifanyia kazi suala la maslahi ya wafanyakazi wa chini ambapo kwa sasa ni madogo sana.

**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

Tume ya Maadili ya Viongozi ni taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria namba 4 ya mwaka 2005 ina mamlaka ya kusimamia Maadili ya viongozi wa Umma ikiwemo kupokea, kusajili na kuhakiki tamko la mali na madeni kutoka kwa viongozi wa Umma, kufanya uchunguzi kuhusu uvunjwaji wa sheria ya maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika ofisi ya Unguja na kugundua changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

1. Udogo wa bajeti
2. Ukosefu wa Ofisi ambapo hadi sasa wanakaa katika jengo la kuazimwa.
3. Ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi.
4. Kamati pia imejuilishwa kuwa kuna Uchache wa wafanyakazi kwa Unguja na Pemba na kwa upande wa Pemba kuna mfanyakazi moja tu hadi sasa.
5. Ukosefu wa usafiri ambapo hadi sasa hawana usafiri kwa Unguja na Pemba na mwenyekiti ana gari ambayo kaazimwa.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri kupatiwa Tume bajeti inayowatosheleza katika kutekeleza kazi zao za kila siku.
2. Kamati inasisitiza kupatiwa ofisi Tume ya Maadili kwani walipo wameazimwa lakini pia mazingira hayaridhishi kutokana na uchakavu wa jengo hilo ambalo wakati wa mvua linavuja.
3. Kamati inaagiza kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi Tume ya Maadili ili waweze kutekeleza kazi zao ipasavyo.
4. Kamati pia inaagiza kupatiwa wafanyakazi kwa upande wa Unguja na Pemba ili waweze kumudu vizuri kazi zao kwani kwa sasa imekua ni mzigo kwa wafanyakazi waliopo na wingi wa kazi zao.

5. Kamati inaitaka wizara kufanya jitihada za makusudi kuwapatia usafiri Tume ya Maadili ili waweze kutekeleza vyema kazi zao.

**KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA**

Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi, chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya Utumishi wa Umma kwa Zanzibar.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA.**

***Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara kwa Kamisheni ya Utumisheni wa Umma na kugundua yafuatayo:-***

1. Kamati imeelezwa kuwa hadi sasa Kamisheni ya Utumishi Umma haina jengo lake la Ofisi na kwa sasa wanakodi jengo la bandari lakini pia ni dogo na halitoshelezi.
2. Pia wa uhaba wa wafanyakazi.
3. Kamati imejuilishwa kuwepo kwa uhaba wa fedha na ucheleweshwaji wa kupatiwa fedha ni kitu ambacho hupelekea baadhi ya malengo kushindwa kutekelezwa.
4. Kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile kompyuta, printa na fotokopi.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri kamisheni kuziangalia Taasisi nyeti za SMZ ambazo zinahitaji kusaidiwa kimaslahi kutokana na kazi zao lakini pia na mazingira magumu ya kazi zenyewe, kama vile ZAECA
2. Kamati pia inaushauri kuangaliwa muongozo wa Utumishi wa Umma kwa watu wenye ulemavu kwa sababu hadi sasa kuna tatizo kubwa la ajira kwa watu wenye ulemavu kitu ambacho kinarudisha nyuma jitihada zinazofanywa na watu hao. Hata hivyo, muongozo huo ueleze mazingira ya kazi kwa watu wenye ulemavu kwa sababu ni lazima ajira ya Mtu mwenye ulemavu iwe rafiki na mazingira.
3. Kamati inaagiza kufanyiwa haraka upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na kuongezwa wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.
4. Kamati pia inashauri kuangaliwa suala la bajeti kwa mwaka ujao wa fedha lakini pia upatikanaji uwe kwa wakati kwani uchelewaji wa fedha za matumizi unasababisha uzorotaji katika kutekeleza majukumu ya kazi.
5. Kamati inashauri kufanyiwa kazi suala la nidhamu kwa wafanyakazi katika maeneo ya kazi ili kuweza kuboresha huduma zinazotolewa na Taasisi za Serikali.

**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

1. Hali ya jengo hairidhishi ni chakavu sana na halina nafasi kitu ambacho kamati imeona ni busara basi Serikali ikawapatia ofisi nyengine.
2. Kutokana na uhaba wa nafasi wameieleza kamati kuwa hadi sasa hawana sehemu maalum ya kuhifadhia nyaraka zao.
3. Kamati imeelezwa hadi sasa Tume haina gari kitu ambacho kinakwaza utekelezaji wa kazi zake. Pia wameieleza kamati kuwa kazi zao zote hadi za kwenda kwenye usaili basi wanatumia daladala.

4. Kwa upande wa Pemba hadi sasa hawana ofisi ila kuna afisa wao mmoja tu ambae anashuhulikia na kuratibu kazi za Tume kwa upande wa Pemba. Pia wameieleza kamati iwapo wanataka kufanya usaili Pemba basi wanatumia wizara ya Katiba au kama usaili utahusu wizara nyengine basi wanakwenda kufanya katika wizara husika kitu ambacho ni changamoto katika utekelezaji wa majukumu yao.
5. Kamati imeelezwa na Tume kuwa wana changamoto ya bajeti kwanza ni ndogo sana ambapo haikidhi haja lakini pia kile wanachokiomba tufauti na wanachoingiziwa.
6. Kamati pia imeelezwa hadi sasa wajumbe wa Tume hawana ofisi na iwapo watakuwa na kazi zao basi inabidi waazimwe ofisi na watumishi wa Tume ambapo hao watumishi basi nao sehemu wanayofanyia kazi haiwatoshelezi.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaomba kuchukuliwa hatua suala zima la kuwapatia ofisi ambayo itakua na nafasi ili waweze kuondokana na changamoto zinazowakabili sasa.
2. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua za haraka kupatiwa usafiri ambao utawasaidia katika kutekeleza kazi zao.
3. Kamati inaomba kuangaliwa suala zima la bajeti ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
4. Kamati inaagiza kupatiwa ofisi kwa upande wa Pemba ili kuepuka chanagamoto zinazojitokeza hivi sasa.

**KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA**

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inaendelea na jukumu la kusimamia mali za wakfu, mali za amana, mirathi ya Waislam,sala na Mabaraza ya Iddi kitaifa, Hijja, Zakka,Sadaka na misaada ya kheri.

**OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI**

Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki ina jukumu la kusimamia matumizi halali ya hakimiliki ili kuhakikisha hali, hadhi na maslahi ya wabunifu wa wasanii yanaimarika. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi za Msajili wa Hakimiliki kwa upande wa Unguja na Pemba ambapo ilibaini yafuatayo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI**

1. Kamati imejuilishwa kwa Ofisi ya Unguja kuna uchache wa wafanyakazi hasa katika kitengo cha leseni ambapo hadi sasa kitengo kina mfanyakazi mmoja.
2. Kamati imejuilishwa kwa upande wa Pemba wana changamoto ya usafiri ambapo hadi sasa hawana gari na inawabidi kutumia gari ya Afisa Mdhamin katika kutekeleza shughuli zao za kazi.
3. Pia kamati imejulishwa kuwa wana ufinyu wa ofisi kwa upande wa Pemba kwani hadi sasa wana chumba kimoja ambacho wanakaa wote hali ambayo inaleta usumbufu katika kufanya kazi zao.
4. Kamati pia imeelezwa kuna tatizo la baadhi ya makampuni kutoa kazi za wasanii kinyume na sheria.
5. Kamati imejuilishwa kuwa kuna tatizo la wasanii kutosajili kazi zao hali ambayo inapelekea upotevu wa mapato.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua suala la upungufu wa wafanyakazi katika kitengo cha leseni kwani utekelezaji wa kazi kwa sasa ni mgumu kutokana na kufanywa na mtu mmoja na kamati inaona hali hii inaweza kupunguza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.
2. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua suala la usafiri kwa upande wa Pemba kwani linakwaza utekelezaji wa kazi zao.
3. Vile vile kamati inashauri kuangaliwa suala la kupatiwa eneo la kufanyia kazi lenye nafasi ya kutosha ambalo litawawezesha kufanya kazi kiufanisi zaidi.
4. Aidha kamati inaagiza kuwachukulia hatua wale wote ambao wanatoa kazi za wasanii kinyume na utaratibu kwa lengo la kukwepa kulipa kodi.

**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ina jukumu la kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho ya sheria hizo,ili ziende sambamba na wakati na mabadiliko ya kisiasa,kijamii na kiuchumi.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TUME YA KUREKEBISHA SHERIA**

1. Wana tatizo la usafiri ambapo hadi sasa wana gari 2 moja ya Mwenyekiti na moja ya wanasheria kitu ambacho kinakwaza katika utekelezaji wa majukumu yao.
2. Kamati imebaini kuna usimamizi mbaya wa utekelezaji wa sheria kitu ambacho kinarudisha nyuma suala zima la utekelezaji wa sheria husika.
3. Ushiriki mdogo wa baadhi ya maafisa wa taasisi mbali mbali wanaohusika na mapitio ya sheria katika kushirikiana na Tume kwa wakati.
4. Kuwepo na ukosefu wa baadhi ya vitendea kazi.
5. Kamati imejuilishwa kuwa kuna uhaba wa vitabu katika maktaba.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kulitilia mkazo suala la Sheria ya Ndoa ya Kiislam ambapo hadi sasa haipo na ni tatizo katika kesi zinazohusu masuala ya ndoa ya kiislam na kupelekea kuwepo ugumu wakati wa kutolewa hukumu.
2. Kamati inaishauri Tume kufanya jitihada za makusudi kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na mambo ya sheria ili ipate uelewa na muamko juu ya mambo ya kisheria hasa katika utafutaji wa haki.
3. Kamati inaiagiza wizara ya katiba kufanya mawasiliano juu ya ushiriki wa maafisa kutoka katika taasisi mbali mbali za Serikali na kuhakikisha wanashiriki katika mapitio ya sheria na Tume ya Kurekebisha Sheria.
4. Kamati inashauri wizara kutenga fungu maalum ambalo litaiwezesha Taasisi kupata vitabu vya kutosha kuweza kukidhi mahitaji Tume.

**MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI**

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ina jukumu la kutoa elimu kwa umma juu ya athari za rushwa na uhujumu uchumi, kufanya udhibiti na utafiti pamoja na kuzishauri Taasisi binafsi na za serikali juu ya namna bora ya kudhibiti mianya ya rushwa

na uhujumu wa uchumi na kufanya uchunguzi dhidi ya vitendo vyote vinavyohusiana na rushwa na uhujumu wa uchumi.

Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mamlaka hii na kubaini changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI**

1. Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa bajeti kwa ZAECA ambayo inawakwaza kutekeleza shughuli zao za kazi.
2. Kuwepo kwa uhaba wa usafiri, ambapo kwa sasa wana gari mbili moja ya Mkurugenzi na moja inatumika kwa ofisi nzima hali ambayo kwa uzito wa kazi zao inakua vigumu katika kutekeleza majukumu yao.
3. ZAECA inakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi vya kisasa hasa vifaa vya kiuchunguzi.
4. Ukosefu wa ofisi ya kudumu pia imeelezwa kuwa ni changamoto kwani walipo sasa nafasi ni ndogo, hakuna sehemu maalum ya kuhifadhia nyaraka muhimu za kazi. Aidha hakuna sehemu maalum kwa watu wa IT ambao wanafanya kazi zao za kiuchunguzi, na usalama wa jengo ni mdogo kwa vile ni la zamani na limeshachoka.
5. Pia ZAECA wana ukosefu wa ofisi kwa upande wa Pemba kwani jengo wanalotumia hivi sasa wamekodi.
6. Kamati imeelezwa kutokuwepo kwa mashirikiano ya wakuu wa idara na taasisi za serikali katika kushiriki kwa dhati kwenye jitihada za kupambana na rushwa.
7. Kamati imeelezwa kuwepo kwa maslahi madogo kwa wafanyakazi wa ZAECA kutokana na mazingira magumu wanayofanyia kazi na unyeti wa kazi zao hali hii hupelekea kuondoka kwa wafanyakazi mara kwa mara.
8. Kamati imeelezwa kuwepo kwa ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi maalum kama (savier, planer, n.k)
9. Kamati imeelezwa kutokana na uhaba wa bajeti inapelekea wafanyakazi wao kukosa mafunzo na kushiriki katika mikutano ya kimataifa inayohusu masuala ya rushwa kwani huwa hawana uwezo wa kwenda na kawaida wanatakiwa wawe na utaratibu wa kupatiwa mafunzo hayo kila baada ya muda kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zao na kwenda sambamba na mbinu za kitaalamu zaidi katika uchunguzi.
10. Wafanyakazi wa ZAECA kukosa usalama katika utekelezaji wa kazi zao ambapo mda mwengine wanakutana na watu hatari.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

**1**. Kamati inashauri kuangaliwa suala la bajeti kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ili waweze kutekeleza kazi zao ipasavyo.
**2**. Kamati inashauri suala la usafiri lipewe kipaumbele kwani linawakwaza katika utekelezaji wa shughuli zao za kazi.
**3**. Kamati inasisitiza kuchukuliwa hatua za kupatiwa ofisi Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ili waweze kutekeleza kazi zao kiufanisi zaidi tofauti na sasa ambapo hali ya jengo ilivyo inawakwaza. vile vile kwa upande wa Pemba nako wizara ijitahidi kuwapatia ofisi ya kudumu Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.
**4**. Kamati inaagiza kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi Mamlaka ili ile dhana iliyokusudiwa iweze kufikiwa.

5. Suala la ushirikiano katika jitihada za kupambana na rushwa kamati inaitaka wizara kuchukua hatua kwa wale wote wasiotaka kutekeleza azma hiyo.
**6**. Kamati pia inashauri kuzingatia maslahi ya wafanyakazi wa ZAECA kwani kazi zao ni nyeti na wanazifanya katika mazingira magumu.
**7**. Kamati inaiagiza wizara kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi maalum katika fani ambazo wanazihitaji katika kutekeleza kazi zao.
**8**. Kamati inashauri kuangaliwa suala la usalama kwa wafanyakazi wa ZAECA kwani kazi zao zinapelekea kuwaweka katika wakati mgumu.

**CHUO CHA UTAWALA WA UMMA.**

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara kwa Chuo cha Utawala wa Umma kwa Unguja na Pemba na kugundua yafuatayo:-

**CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI CHUO CHA UTAWALA WA UMMA**

1. Kwa upande wa Chuo Cha Utawala wa Umma Pemba kamati imegundua kuwa kuna tatizo la ukosefu wa jengo la chuo kwani hadi sasa wanakaa katika jengo la kukodi kitu ambacho kinakua ni mzigo kwa chuo.
2. Kamati imegundua Chuo kina changamoto ya uhaba wa fedha za kuendeshea Lakini pia hadi leo chuo hakina hata account jambo amabalo linatia mashaka katika matumizi ya fedha za Serikali.
3. Kamati imeelezwa kuwa chuo hakina usafiri hadi leo wana vespa moja tu ambapo ni changamoto katika utekelezaji wa kazi za chuo.
4. Vile vile chuo kina mfanyakazi aliyeajiriwa mmoja tu ambae kama mwalimu lakini pia yeye ndo sekretari kitu kinachokwaza utekelzaji wa kazi hizo.
5. Kamati imejuilishwa kwa upande wa Unguja chuo kina changamoto ya kupungua idadi ya wanafunzi kutokana na ushindani wa vyuo vilivyopo nchini.
6. Kamati imejuilishwa pia kuna baadhi ya Taasisi na Wizara za Serikali hazilipi madeni ya wanafunzi wao wanaowasomesha kupitia chuo hicho hali amabyo inasababisha kupunguza ufanisi wa uendeshaji wa chuo.
7. Kamati imegundua chuo cha IPA Unguja hakina uzio kitu ambacho kinahatarisha usalama wa chuo.

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri katika kupambana na tatizo la uhaba wa wanafunzi chuo kifanye utafiti ili kujua chanzo cha tatizo na kuweza kutoa elimu iliyo bora.
2. Kamati inashauri Serikali kutumia chuo hiki cha IPA kufanya tafiti mbali mbali za kitaaluma ili kiweze kutambulikana pamoja na kupata hadhi kitaifa.
3. Kamati inaagiza Wizara zote za Serikali ziwe na bajeti za kusomesha watumishi wao kama sheria ya Uajiri inavyoelekeza.
4. Kamati inashauri katika bajeti inayokuja Chuo kizingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kuboresha miundombinu ya majengo ili iweze kuwa rafiki kwao.
5. Vile vile kamati inaagiza chuo kuajiri wakalimani ambao watasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa uziwi.

6. Kamati inashauri kuanzishwa usafiri wa chuo wa kuwasaidia wanafunzi kwani hadi sasa hawana usafiri wa uhakika jambo ambalo litasaidia kupunguza usumbufu kwa wanafunzi.
7. Kamati inashauri kuangaliwa suala la kupatiwa jengo la Chuo kwa upande wa Pemba ili kupunguza gharama za fedha kwa ajili ya kukodi.
8. Kamati inaagiza kuajiriwa wafanyakazi wa chuo kwa tawi la Pemba ili chuo kiweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

**MAONI NA MAAGIZO YA JUMLA YA KAMATI KWA WIZARA YA KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

1. Kuanzishwa Ofisi zisizokuwepo kwa upande wa Pemba.
2. Kamati inaagiza kufanyiwa matengenezo ya majengo ya mahkama kwa Unguja na Pemba.
3. Kamati inasisitiza kuwepo kwa mashirikiano kati ya Ofisi ya DPP, Polisi, Mahkama na jamii katika kuleta ufanisi wa uendeshaji wa kesi.
4. Katika suala la watumishi wa Serikali wanaostaafu kuongezwa mda kamati inaiomba Serikali itamke rasmi kada maalum ambazo zinafaa kuongezewa mda watumishi wake wanapostaafu.
5. Kuchukuliwa hatua za ununuzi wa vifaa katika idara na Taasisi za Serikali ili ziweze kufanya kazi vizuri.

## SEHEMU YA TATU

**WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**

Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na kusimamiwa ni Idara na Taasisi mbali mbali zilizogawika maeneo makuu manne katika kutimiza majukumu yake pamoja Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Aidha, Kamati inaiponeza sana Serikali kwa kuweza kuwapatia fungu lao la bajeti kwa asilimia kubwa katika Taasisi na Idara zake zote tofauti na miaka ya nyuma.

Idara na Taasisi hizo zimegawika kama ifuatavyo:-

**A) IDARA ZA KAWAIDA**

1. Idara ya Mipango Sera na Utafiti;
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
3. Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ;
4. Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
5. Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho;
6. Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo.

**B) MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA**

1. Mkoa wa Mjini Magharibi,
2. Mkoa wa Kusini Unguja,
3. Mkoa wa Kaskazini Unguja

4. Mkoa wa Kusini Pemba, na
5. Mkoa wa Kaskaznini Pemba.

**C) MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA**

1. Baraza la Manispaa ya Mjini,
2. Baraza la Manispaa ya Magharibi ‘A’
3. Baraza la Manispaa ya Magharibi ‘B’
4. Baraza la Mji – Wete,
5. Baraza la Mji – Chake Chake,
6. Baraza la Mji – Mkoani,
7. Wilaya ya Mjini – Unguja,
8. Wilaya ya Magharibi ‘A’
9. Wilaya ya Magharibi ‘B’
10. Halmashauri ya Wilaya ya Kusini – Unguja,
11. Halmashauri ya Wilaya ya Kati,
12. Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini ‘A’
13. Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini ‘B’
14. Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani,
15. Halmashauri ya Wilaya ChakeChake,
16. Halmashauri ya Wilaya ya Wete, na
17. Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

**D) IDARA MAALUM ZA SMZ**

1. Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ,
2. Tume ya Utumishi Idara Maalum za SMZ,
3. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)
4. Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)
5. Chuo cha Mafunzo,
6. Kikoksi cha Zimamoto na Uokozi,
7. Kikosi cha Valantia (KVZ)

**A) IDARA ZA KAWAIKA**

**1. IDA YA MIAPANGO SERA NA UTAFITI**

Idara ya Mipango sera na Utafiti ndio kiungo baina ya Taasisi za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na wizara na Taasisi nyengine zinazoratibu masuala mbali mbali. Jukumu kubwa la Idara hii ni kuratibu utekelezaji wa shughuli za kila siku za Idara na Taasisi za Wizara katika masuala ya Mipango, Sera na Utafiti.

**2. IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

Idara ya uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kutoa na kusimamia huduma za uendeshaji na Utumishi katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, zikiwemo kusimamia sheria na kanuni zinazosimamia utumishi na uendeshaji wa Ofisi, kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kusimamia utumishi na vitendea kazi na kuendelea na kusimamia utunzaji wa kumbukumbu.

3. **IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM WA SMZ**
   Kamati imeelezwa kuwa Idara ya Uratibu wa Idara Maalum wa SMZ ina jukumu la kuratibu na kusimamia kazi za Idara Maalum za SMZ zikiwemo za utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za Idara Maalum na kusimamia vikao vya Mahkama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ.

   Vile vile, Kamati imeelezwa kuwa Idara hii ina jukumu la kisera, kusimamia mwendo wa kiutumishi, maslahi ya maafisa na wapiganaji, kuratibu masuala ya michezo pamoja na mashirikiano na vyombo vya ulinzi ndani na nje ya nchi.

4. **IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
   Idara ya uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kutoa miongozo kwa Taasisi za Mamlaka na Serikali za Mitaa. Katika kufanikisha majukumu yake inasimamia utkelezaji wa maagizo ya mipango mikuu ya Serikali, sera za Serikali na kusimamia utekelezaji wa sheria Nam. 7/2014 ya Serikali za Mitaa na sheria Nam.8/2014 ya Tawala zaMikoa.

5. **OFISI YA MRAJISI WA VIZAZI NA VIFO**
   Afisi ya Mrajisi wa vizazi na vifo ina dhima ya kisheria ya kusajili vizazi na vifo pamoja na kutunza kumbukumbu zinazotokana na usajili huo. Vile vile, afisi hii inawajibika kuishauri Serikali kuhusu masuala ya usajili wa vizazi na vifo, kutoa mafunzo yanayohusiana na usajili kwa watendaji na wakala wa usajili pamoja na jamii kuhusu masuala ya usajili wa vizazi na vifo.

   **Changamoto za Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo:**

1. Kamati imeelezwa kuwa tabia ya wananchi ni kujisajili zaidi katika vizazi na ndoa lakini jamii haina mwamko kujisajili katika vifo na talaka, suala ambalo ni changamoto nzito ya ofisi hii katika kujikusanyia mapato yake.
2. Kuwepo kwa changamoto ya ucheleweshwaji na utolewaji wa veti vya kuzaliwa, hivyo kupelekea baadhi ya wananchi kuacha kuvifuatilia baada ya kukaa kwa muda mrefu.
3. Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la mashekhe kutorejesha vitabu vya malipo baada ya kufungisha ndoa.

   **Maoni na Magizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujisajili katika vyeti vya kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka.
2. Kamati inaagiza ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kuhakikisha vyeti vinapatikana kwa wakati unaotakiwa bila ya kuchelewa na hivyo wananchi kupata haki yao ya msingi kwa wakati.
3. Kamati inaagiza kuwa utaratibu wa utoaji wa vitabu vya vyeti vya ndoa vilipiwe mwanzo na wahusika badala ya kuverijesha wakati wanapo maliza kutumia.

B) **<u>MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA</u>**
   Katika ziara zake za kawaida Kamati ya Sheri, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi, iliweza kuzitembelea Taasisi mbali mbali za Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na kujionea mambo

kadhaa ambayo yanarudisha nyuma juhudi za watendaji wake. Hivyo, Kamati ilifanikiwa kuzitembelea Taasisi tofauti za wizara hii kama ifuatavyo:-

**MKOA WA MJINI MAGHARIBI**

Mkoa wa Mjini Magharibi ni miongoni mwa mikoa yenye kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu yake katika kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuzingatia makundi mbali mbali yaliyomo katika jamii. Ofisi imeendelea na jukumu lake la kusimamia ulinzi na usalama kwa raia na kuhakikiksha kila mmoja anaishi kwa usalama na amani.

**Changamoto za Mkoa wa Mjini Magharibi:**

1. Kamati imeelezwa kuwepo kwa migogoro ya ardhi katika Mkoa huu, ambayo ipo migogoro baina ya raia kwa raia na migogoro baina ya raia na Serikali.
2. Kamati imeelezwa kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa vituo vya parking katika maeneo mjini na sehemu zenye kutolewa huduma za kijamii.
3. Kuwepo kwa ongezeko la tatizo la kesi za ubakaji na udhalilishaji kwa watoto na watu wenye ulemavu. Kamati imesikitishwa kuona kuwa kila siku kesi hizi zinazidi kuongezeka na imekuwa suala la kawaida kwa wananchi kusikika katika vyombo vya habari bila jamii kuzingatia kuwa inaelekea kupotea.
4. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kwa Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na Manispaa zake imekuwa ni kikwazo kikubwa katika kuleta ufanisi wa utendaji.
5. Vile vile, imeelezwa kuwa ukosefu wa majengo ya ofisi za serikali ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoukabili Mkoa huu na hivyo kupelekea baadhi ya ofisi muhimu za Serikali kukodi majengo ya raia.
6. Kamati imebaini kuwepo na tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika sehemu nyingi za Mkoa wa Mjini Magharibi.
7. Kamati imeelezwa kuwepo kwa ongezeko kubwa la matumizi ya madawa ya kulevya kwa Mkoa wa Mjini Magharibi hususan kwa vijana wenye umri mdogo.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri uongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na Taasisi husika kuhakikisha wamesimamia migogoro yote ya ardhi na kusuluhishwa kwa mujibu wa taratibu na kuzingatia haki za wahusika.
2. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua zinazostahiki watu wanaolaza magari katika barabara zote za Mkoa wa Mjini Magharibi wakati wa usiku kwani imekuwa ni tatizo kwa watumiaji wa barabara hiyo;
3. Kamati inaagiza uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi kuhakikisha wanakomesha vitendo vya udhalilishaji na ubakaji kwa watoto na watu wenye ulemavu ili kutoa fursa sawa ya kuishi kwa salama na amani;
4. Kamati inaishauri Serikali ya Mkoa kuwa vituo vyote vya parking za magari vilivyopo mjini ni bora kubinafsishwa na mamlaka husika kukusanya kodi kupitia kwa wamiliki wa parking hizo,
5. Aidha, Kamati inaiagiza Serikali kuharakisha ujenzi wa kituo kikuu cha Daladala cha Kijangwani. Vile vile Kamati hairidhiki kuwepo kwa kituo cha Daladala mbele ya ofisi kuu ya CCM Kisiwandui mpaka Tobo la Pili Michenzani, hivyo Kmati inashauri kuondolewa kwa kituo hicho.

6. Vile vile, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha suala la uhaba wa Majengo ya Ofisi za Serikali limepatiwa ufumbuzi ili kuepuka kukodi majengo kila siku kwa ajili ya ofisi na kutumia pesa nyingi za Serikali kwa kulipia gharama za kodi hizo;
7. Kamati imeagiza kudhibitiwa kwa majitaka katika barabara kuu inayoingia airport Zanzibar ili kuweka mji safi na haiba mzuri kwa wageni wanaoingia kila siku.
8. Kamati inaagiza uongozi wa Mkoa wa Mjini kwa kushirikiana vyombo vya ulinzi kuhakikisha kwamba suala hilo la madawa ya kulevya linapigwa vita kwa nguvu zote.

**MKOA WA KUSINI – UNGUJA**

Mkoa wa Kusini – Unguja umefanikiwa kufuatilia shughuli zake mbali mbali za kimaendeleo ikiwemo huduma za kiafya, elimu, maji, kilimo na shughuli mtambuka kwa vijana. Aidha, umewajengea uwezo watendaji wake kwa kuwapatia mafunzo ya sheria ya utumishi pamoja na vikao mbali mbali vya kujadili usalama wa raia wa mkoa huu.

**Changamoto za Mkoa wa Kusini – Unguja:**

1. Ufaulu mdogo kwa wanafunzi katika mitihani ya darasa la saba, kidato cha pili na cha nne, Kamati imeelezwa kuwa chanzo cha ufaulu mdogo wa wanafunzi katika Mkoa huu ni utoro wa wanafunzi uliokisiri kwa skuli zote za msingi na sekondari.
2. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa vikundi vya ushirika vinakabiliwa na changamoto nyingi kama vile ukosefu wa elimu ya uendeshaji pamoja na ukosefu wa fedha.
3. Ongezeko la kesi za udhalilishaji na ulawiti. Kamati imeona kuwa kumekuwa na idadi kubwa ya kesi za udhalilishaji katika Mkoa wa kusini Unguja ambapo waathirika wakubwa ni watoto na watu wenye ulemavu.
4. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa matumizi ya bandaribubu ambazo zinanyima kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato na kutia hasara serikali.
5. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwa kuna baadhi ya majengo ya Serikali katika Mkoa huu hayana Hatimiliki.

**Maoni na Maagizo ya Kamati kwa Mkoa wa Kusini – Unguja:**

1. Kutokana na athari kubwa za matukio ya kesi za udhalilishaji na ubakaji, Kamati inashauri Serikali na Taasisi zinazohusika kusimamia sheria kuchukua hatua kali katika kudhibiti tatizo hili ili iwe funzo kwa watendaji na wahalifu wengine wenye kufanya vitendo kama hivi.
2. Aidha, Kamati inashauri kuendelezwa kwa mabaraza ya vijana ili kuwawezesha vijana kupambana na mazingira yaliyowazunguka kifikra na kiuchumi ili kuachana na mawazo potofu ambayo ni kikwazo cha maendeleo.
3. Kamati vile vile, inaagiza Mkoa wa Kusini kusimamia kikamilifu ongezeko la matumizi ya bandari bubu ili kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya rasilimali za Serikali.
4. Kamati imeagiza Mkoa wa Kusini Unguja kufanya tathmini na kujua idadi ya maeneo na majengo ya ofisi za Serikali ambayo hayana Hatimiliki na kuyatafutia kwa mujibu wa taratibu za idara husika.
5. Kamati inashauri juhudi za pamoja zifanyike kati ya wazazi, walimu na uongozi wa Mkoa katika kunyanyua hali ya elimu kwa Mkoa huu.

**MKOA WA KASKAZINI – UNGUJA**

Kamati imeelezwa kuwa ofisi ya Mkoa imeendelea na kufanya shughuli zake za kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta mbali mbali za kijamii kama vile maji, elimu, afya, kilimo na mazingira, watu wenye ulemavu, wanawake na watoto na ustawi wa jamii. Aidha, Mkoa umefuatilia migogoro ya ardhi iliojitokeza katika maeneo ya Donge Pwani, Donge Mchangani na Kinyasini. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwa Mkoa huu uko mstari wa mbele katika kusimamia hali ya ulinzi na usalama kwa wananchi wake.

Licha ya mafanikio hayo, Kamati imesikitishwa sana kwa kuona ongezeko kubwa la kesi za udhalilishaji na ubakaji kwa watoto na watu wasiojiweza kwa Mkoa huu na hivyo kurudisha nyuma juhudi za kupinga vitendo hivi vya udhalilishaji na ukatili.

**Changamoto za Mkoa wa Kaskazini – Unguja:**

1. Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hiki, Kamati imeelezwa kuwepo kwa changamoto ya kesi za udhalilishaji na ukatili zikiwaathiri zaidi wanawake na watoto. Aidha, Kamati imeelezwa kuwa katika kukabiliana na changamoto hii Mkoa umebuni njia mbali mbali za kupinga vitendo hivi kamavile:-

   i. Kuundwa kwa kamati za kumlinda mtoto;
   ii. Kutolewa uwelewa kwa wanajamii juu ya athari za matendo haya;
   iii. Kutolewa ushauri nasaha kwa waathirika wa vitendo hivi; na
   iv. Kuanzishwa kwa dawati la watoto ili kupewa taaluma ya kujikinga na vitendo viovu dhidi yao.

2. Hata hivyo, Kamati imeshangazwa kuona kuwa katika Mkoa huu hakuna takwimu halisi ya wageni (watalii) wanaoingia kwa mwaka mzima jambo ambalo linaashiria upotevu wa mapato ya Serikali kwa wahusika kutokuweka takwimu sahihi za wageni.
3. Kamati pia, kwa kufanya mahojiano na watendaji wa Mkoa, imeelezwa kuwa maendeleo ya elimu kwa Mkoa huu ni mabovu na mara zote hushikilia nafasi za mwisho katika matokeo ya mitihani ya kitaifa. Hivyo, inadaiwa kuwa chanzo cha matokeo hayo ni mwamko mdogo wa jamii, utoro, uhaba wa walimu katika masomo ya sayansi na hisabu pamoja na vifaa vya kufundishia.
4. Vile vile, Kamati imeelezwa kuhusu tatizo la uhaba wa usafiri kwa Mkoa huu katika ngazi mbali mbali za kiutawala na utendaji.
5. Ukosefu na uchakavu wa vitendea kazi katika harakati za kila siku, pia imeelezwa kuwa ni changamoto zinazoukabili Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa watumishi na maafisa wake.
6. Kamati imebaini kuwepo kwa matamasha na madisko mengi ya starehe (mfano kuwepo kwa full moon party kila mwezi) katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ambako kunachangia kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji na utumiaji wa madawa kulevya.

**Maoni na Maagizo ya Kamati kwa Mkoa wa Kaskazini – Unguja:**

1. Katika kusimamia ukosefu wa takwimu za data sahihi za wageni wanaoingia katika Mkoa huu, Kamati inaagiza uongozi wa Mkoa wa Kaskazini kupitia ofisi yake inayoshughulikia utalii kutafuta na kuweka takwimu halisi za watalii wote wanaoingia katika Mkoa huu ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

2. Kama ilivyo Mikoa mengine, katika Mkoa huu pia, Kamati imeagiza Serikali ya Mkoa kusimamia kesi za udhalilishaji na ubakaji na kuhakikisha kuwa watuhumiwa wanachukuliwa hatua zinzofaa, baada ya kuona kuwa katika Mkoa wa Kaskazini kesi hizi zimezidi licha ya jitihada nyingi zinazochukuliwa na Serikali ya Mkoa kwa kuwapa elimu wananchi wake.
3. Aidha, Kamati inashauri kusimamiwa vyema suala la maendeleo ya elimu katika Mkoa huu kwa kupatiwa vifaa vya kujikfunzia pamoja na kupatiwa walimu wa kutosha katika masomo ya sayansi na hesabati.
4. Vile vile, Kamati inaishauri Serikali na wizara kufanya jitihada za makusudi katika kuhakikisha kuwa imewapatia vitendea kazi watendaji wa Mkoa huu ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.
5. Kamati inaishauri Serikali ijiangalie na kujitathmini kama zoezi hilo la kuzidi kwa shughuli za starehe linafaida kwa wananchi wa Mkoa huo?

**MKOA WA KASKAZINI – PEMBA**

Kamati imeipongeza sana Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kusimamia vyema suala la usalama kwa kipindi chote cha uchaguzi wa 2015 pamoja na uchaguzi mdogo wa marudio wa mwezi wa machi 2016. Katika kusimamia utekelezaji mzuri wa majukumu yake, Kamati imeipongeza kwa kutumia vyema fedha za matumizi ya Afisi ambapo wameingiziwa zaidi ya asilimia 98 kwa mujibu wa fedha ya matumizi waliyoomba. Aidha, Kamati inapongeza uongozi wa Mkoa kwa kupiga marufuku uoneshaji wa TV maeneo ya wazi katika kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji.

**Changamoto za Mkoa wa Kaskazini – Pemba:**

1. Kamati imeelezwa kuwa katika Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna tatizo la uhaba wa wafanyakazi zaidi ya 10 kwa upande wa afisi ya Mkoa, afisi ya wilaya ya Wete 4 na afisi ya Wilaya ya Micheweni 6.
2. Pia, Kamati imeelezwa kuwa suala la udhalilishaji wa watoto na watu wenye ulemavu lipo ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba na hatua mbali mbali zinachukuliwa kukabiliana na watendaji wa kesi hizo, kama vile kufanya mikutano ya kidini ili kupunguza tatizo hili, sambamba na hili kwa upande wa watumishi wa SMZ na wale wa Serikali ya Muungano hatua watakazo chukuliwa pindi wakigundulika na vitendo hivi watapatiwa uhamisho kutoka Mkoa huu.
3. Kamati imeelezwa kuwa Afisi ya Mkoa imetumia Redio jamii Micheweni kurusha vipindi vya *live* kwa lengo la kuielimisha jamii kutokana na vitendo hivi vya udhalilishaji na ukatili.
4. Kwa upande mwengine, Kamati imeelezwa kuwa vitendo hivi huongezeka siku hadi siku kutokana na suluhu zinazofanywa na kuoneana aibu kwa wanajamii wenyewe bila ya kuwapeleka wahusika wa vitendo hivyo katika vyombo vya sheria.
5. Pia, Kamati imesikitishwa na kuwepo kwa tabia iliyojitokeza hivi karibuni kwa baadhi ya wananchi kuharibiwa vipando vyao kutokana na chuki za kisiasa.

**Maoni na Maagizo ya Kamati kwa Mkoa wa Kaskazini – Pemba:**

1. Kamati inashauri Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kuandaa mpango maalum wa kuwafanyia uchunguzi mara kwa mara watoto wa shule za msingi na madrasa za Quran

ili kubaini ongezeko la tatizo la udhalilishaji na ulawiti na kulichukulia hatua zinazofaa kwa haraka inavyowezekana.

2. Kamati inashauri Serikali ya Mkoa kuzingatia mahitaji ya msingi kwa watu wenye ulemavu wakati wanapotoa misaada ya kijamii na kiuchumi.
3. Kamati inaagiza Afisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kutoa taarifa kamili pamoja na idadi ya matukio yote ya kesi za udhalilishaji kwa kipindi cha mwaka huu na kuwachukulia hatua kali za kisheria watumishi wa Serikali wanaobainika kuendeleza matukio ya udhalilishaji katika jamii.
4. Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kukomesha vitendo vya baadhi ya wananchi wenye tabia ya kuharibu mazao ya wakulima kutokana na chuki za kisiasa.

**MKOA WA KUSINI – PEMBA**

Mkoa wa Kusini Pemba ni kiungo muhimu sana cha kuchangia mapato ya Serikali kupitia Mabaraza yake ya miji ya Ckake Chake na Mkoani. Mkoa huu umefanikiwa sana katika kusimamia ulinzi na usalama wa raia wake pamoja na kuboresha maisha halisi ya wakaazi wake kwa kuwapatia huduma zote muhimu anazostahiki raia wa kawaida kama vile maji, afya bora, elimu, umeme na barabara. Pia, Mkoa umeendelea kuratibu na kusimamia majukumu ya sekta mbali mbali ambazo zimo ndani ya Mkoa huu.

**Changamoto za Mkoa wa Kusini – Pemba:**

1. Ukosefu na uchakavu wa vyombo vya usafiri. Kamati imeelezwa kuwepo kwa uchakavu mkubwa wa gari la Mkuu wa Mkoa pamoja na kushindwa kabisa kufanyakazi kwa gari la Katibu Tawala.
2. Ukosefu wa nyumba za viongozi wa Mkoa na Wilaya. Kamati imeelezwa kuwa kuna ukosefu mkubwa wa nyumba za viongozi kwa Mkoa wa Kusini Pemba na kupelekea kwa viongozi hao kulazimika kupanga nyumba za watu binafsi jambo ambalo linawagharimu fedha nyingi za Serikali.
3. Ukosefu wa wafanyakazi wataalamu kama vile wahandisi majenzi, barabara na afisa Tehama, pia imeelezwa kuwa kikwazo cha miradi ya maendeleo katika Mkoa wa kusini Pemba.

**Maoni na Maagizo ya Kamati kwa Mkoa wa Kusini Pemba:**

1. Kamati inashauri kwa wakuu wa Mabaraza Pemba kuajiri kwa muda wataalamu kwa mikataba kwa mujibu wa mahitaji yao yalivyo kama wanavyofanya Unguja.
2. Kamati inashauri uongozi wa Mkoa kusimamia vyema mabaraza katika kutumia vyema fedha za maendeleo pamoja na zile za mfuko wa Jimbo kwa mashirikiano na wabunge na madiwani.
3. Vile vile, Kamati imeshauri Serikali ya Mkoa kwa kushirikiana na Baraza la Mji Chake-Chake kuajiri Mhandisi wa Ujenzi kutokana na miradi mikubwa ya ujenzi inayofanyika katika Mkoa huu.
4. Kamati imeona kuwa Mabaraza ya miji Pemba yameshindwa kukushanya kodi zake vizuri kutokana na kutozishirikisha Mahakama, hivyo wafanya biashara kupata fursa ya kukwepa kulipa kodi, Kamati inashauri kuwepo kwa mashirikiano mazuri katika Mabaraza na Mahakama kutahamasisha pia upatikanaji wa kodi unaokusudiwa.

## E) <u>MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA</u>

Katka ziara iliyofanywa na Kamati katika Mabaraza na Halmashauri mbali mbali imepata kujonea mambo kadhaa ambayo yanarudisha nyuma juhudi za maendeleo. Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi wataalamu na vitendea kazi katika maeneo yote ya Mabaraza na Halmashauri jambo ambalo ni kikwazo kikubwa cha maendeleo katika Taasisi hizo. Aidha, ukusanyaji mdogo wa mapato katika Taasisi hizi pia unachangiwa ni uhaba wa wafanyakazi wenye sifa za kutosha katika ukusanyaji wa mapato.

Vile vile, katika kukabiliana na uuzaji wa ardhi kiholela, Kamati inashauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuchaguwa Masheha kuandaliwa utaratibu maalumu wa kuzingatia sifa nzuri ya utunzaji wa ardhi na mazingira.

**BARAZA LA MANISPAA**

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ilifanya ziara katika Baraza la Manispaa ya Mjini na kuelezwa kuwa kwa mwaka fedha 2016/2017 Baraza limejipangia malengo ya kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuimarisha huduma za usafi wa mji, kusimamia na kuendeleza maeneo wazi, bustani pamoja na ukarabati wa michirizi na uendelezaji wa taa za barabarani. Aidha, Baraza lilipanga kuweka mazingira bora ya utendaji kazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa stahiki za wafanyakazi na vitendea kazi.

**Changamoto za Baraza la Manispaa ya Mjini:**

1. Kamati imeelzwa kuwepo kwa changamoto ya ukosefu wa vijana kazi ambapo waajiriwa wengine wapo katika utendaji wa chini kutokana na ufinyu wa elimu zao na uzee;
2. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwepo kwa upungufu wa wataalamu katika fani mbali mbali kama vile mtakwimu, afisa manunuzi na mkandarasi;
3. Pia Kamati imeelezwa kuwa kuna muingiliano mkubwa wa kanuni za ukusanyaji wa mapato kwa mfano TRA, ZARB na Mamlaka ya Mji Mkongwe;
4. Aidha, Kamati imeelezwa kuwepo kwa deni kubwa la ZECO ambalo lipo kwa mda mrefu na linarudisha nyuma maendeleo ya Manispaa hii;
5. Hata hivyo, kuwepo kwa changamoto za maslahi madogo kwa watumishi, ukosefu wa ajira za madereva wa manispaa na uhaba wa vitendea kazi, pia imeelezwa kuwa ni kikwazo cha maendeleo ya manispaa ya mjni.

**Maoni na maagizo ya Kamati kwa Baraza la Manispaa ya Mjini:**

1. Kamati inashauri uongozi wa Manispaa kwa kushirikiana na uongozi wa ZECO kukaa pamoja na kutafuta njia sahihi ya kulipatia ufumbuzi suala la deni lililopo katika Baraza la Manispaa ya Mjini,
2. Kamati inaagiza Baraza la Manispaa ya Mjini kuajiri wataalamu katika sekta mbali mbali za kiutumishi ili kuweza kukamilisha malengo yao katika ukusanyaji wa mapato.
3. Vile vile Kamati inashauri kuboreshwa kwa maslahi ya wafanyakazi wa Mabara ya Manispaa, hii itaongeza ari na hamasa katika kukamilisha majukumu ya watumishi.

**BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI ‘A’ NA ‘B’**

Manispaa ya Magharibi A na B ni mpya ambazo zinatokana na Halmashauri ya Magharibi ambazo zilikuwepo miaka ya nyuma, hivyo uwepo wa manispaa hizo mpya

kunailazimisha Seriakli kuzisaidia kwa kuwapatia watumishi wenye uwezo na kuwapatia vitendea kazi ili kujiimarisha katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kamati imeelezwa kuwa Baraza la Manispaa ya Magharibi 'A' na 'B' yalijipangia malengo tofauti kwa mwaka huu katika utekelezaji wake wa Bajeti kama vile kusimamia vyanzo vyake vya mapato na ukusanyaji wa mapato, kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuongeza uzoaji wa taka katika maeneo mbali mbali ya mijini, kusimamia na kuelekeza miradi ya maendeleo na kusimamia uendeshaji wa ofisi.

**Changamoto za Baraza la Manispaa ya Magfharibi 'A' na 'B':**

1. Kamati imeelezwa kuwepo kwa ukosefu wa wafanyakazi wataalamu wa fani mbali mbali kwa mujibu wa majukumu yao ya kazi;
2. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi.
3. Kamati imeelezwa katika Manispaa zote Magharibi 'A' na 'B' kuna tatizo kubwa la kuwepo kwa wafanyakazi wa Daily Pay na hulazimaka kuwalipa kwa mwezi kakriban Tshiling Milioni 24 kwa ujumla wao.
4. Aidha katika Manispaa ya Magharibi A, Kamati imeelezwa kuwa jengo la Hospitali ya Mbuzini limetelekezwa kwa mda mrefu bila kuendelezwa katika ujenzi.
5. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo kubwa la barabara za ndani kwa Manispaa zote za Magharibi A na B na kupelekea kuwa kero kwa watumiaji wa bara bara hizo katika shughuli zao za kila siku.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri katika kusimamia suala zima la ukusanyaji wa mapato basi fursa za kiuchumi ni bora kusimamiwa vyema kwa manispaa zote A na B ili kuziba mianya ya upotevu wa mapato.
2. Vile vile, Kamati inshauri kuimarishwa kwa vitendea kazi ili kujenga mazingira bora ya kazi pamoja na kuongeza ufanisi na ubora wa kiutendaji.
3. Aidha, Kamati inashauri Baraza la Manispaa ya Magharibi 'A' kulisimamia eneo la ujenzi wa Hospitali ya Mbuzini kwa kulipatia Hatimiliki na kulitafutia wafadhili kwa ajili ya ujenzi wa kituo.
4. Kamati inaishauri Serikali kuu kuzisaidia Manispaa hizi katika ujenzi wa Barabara za ndani kwa vile bado ni Manispaa mpya.

**BARAZA LA MJI WETE**

Kmati imeelezwa kuwa Baraza la Mji Wete lina lengo la kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kasi zaidi ili kutofautisha na ukusanyaji mdogo uliopatikana mwaka jana kutokana na harakati za kisiasa na ujenzi wa soko jipya la Wete, vile vile kuimarisha shughuli za usafi kwa mji wa Wete, kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na maslahi ya wafanya kazi pamoja na kuendeleza miradi ya jamii kwa Wadi zake zote za Baraza hilo.

**Changamoto za Baraza la Mji Wete:**

1. Kamati imeelezwa kuwa Baraza halijakusanya mapato yake inavyostahiki licha ya kuongezewa vyanzo vya mapato kutoka Wilaya ya Micheweni, hii inadaiwa ni kutokana na changamoto za wafanyabiashara kushawishiwa ni wanasiasa ili wasilipe kodi.
2. Ukosefu wa wataalamu kwa mfano hakuna Mhandisi, Afisa Tehama na Afisa Majenzi.

3. Ukosefu wa vitendea kazi kama vile makontena ya kukusanyia taka na magari ya upakiaji majitaka.

**Maoni na Maagizo ya Kamati kwa Baraza la Mji Wete:**

1. Licha changamoto hizo, Kamati inashauri kwa watendaji wa Baraza la Mji kuwa waadlifu sana katika suala zima la ukusanyaji wa mapato kwa kuziba mianya yote inayopelekea upotevu wa mapato na kuipa hasara Serikali.
2. Kamati inaishauri Serikali iwe na utaratibu wa kuwapima wakusanyaji wa mapato uwezo wao wa kukusanya mapato na iwapo watagundulika wameshindwa kukusanya mapato basi waondolewe katika maeneo yao ya kazi.
3. Vile vile, Kamati inashauri Baraza la Mji Wete kuajiri wataalam wa fani mbali mbali wanao wahitaji kwa njia ya mkataba ili kufanikisha azma yao katika kunyanyua ukusanyaji wa mapato.
4. Kamati inashauri Baraza kulitumia vizuri soko jipya la Wete katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, Kamati inapendekeza kujengwa uzio wa kutenganisha baina ya ofisi na soko ili kuondoa msongamano kwa watumiaji wa soko hilo.

**BARAZA LA MJI CHAKECHAKE**

Kamati imefanya ziara katika kutembelea miradi mbali mbali ya kimaendeleo ambayo imepangwa kufanyika katika Baraza la Mji ChakeChake, Kamati imefika katika mradi wa ujenzi wa ngazi na vidaraja wa Machomane, mradi wa ujenzi wa soko la matunda na mboga mboga lililopo Mavambaruku na ujenzi wa ofisi ya Baraza la Mji ChakeChake ambao unakaribia kukamilika.

**Changamoto za Baraza la Mji ChakeChake:**

1. Ukosefu wa wafanyakazi wataalamu kama vile wahandisi wa ujenzi na afisa Teknolojia wa habari na mawasiliano.
2. Ukosefu na uchakavu wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati:**

1. Kamati inashauri baraza kutumia vyema fedha za maendeleo pamoja na zile za mfuko wa Jimbo kwa mashirikiano na wabunge na madiwani.
2. Pia, Kamati inashauri kufanyika utaratibu kwa Baraza la Mji ChakeChake wa kuajiri Mhandisi wa ujenzi kutokana na miradi mikubwa ya ujenzi inayofanyika katika maeneo ya mjini.
3. Kamati inaagiza Baraza la Mji ChakeChake kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wanatekeleza agizo la ulipaji kodi ili kuweza kufanikisha malengo yao katika ukusanyaji wa amapato.

**BARAZA LA MJI MKOANI**

Katika ziara iliyofanywa na Kamati kwa Baraza la Mji Mkoani imeelezwa kuwa kwa mwaka huu Baraza limepangiwa malengo makuu manne ambayo ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuimarisha usafi wa mji pamoja na kuimarisha mazingira bora ya kazi.

Aidha, Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi ya maendeleo ya ujenzi wa ngazi na vidaraja iliyochini ya usimamizi wa mradi wa ZUSP katika maeneo tofauti katika mji wa Mkoani ambapo imeridhika na kazi nzuri ya ujenzi huo.

**Changamoto za Baraza la Mji Mkoani:**

1. Kamati imeelezwa kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi wataalamu kama vile muhandisi ujenzi, afisa Tehama, mkaguzi wa hesabu za ndani na afisa habari.
2. Vile vile Kamati imeelezwa kuwepo kwa ugumu wa wafanya biashara kuhamasika juu ya ulipaji wa kodi kwa hiari.
3. Pia, Kamati imeelezwa kuwa baadhi ya wananchi wanatumia vibaya miundo mbinu ya maji ya mvua na kuzuia juhudi za Baraza katika kufanikisha malengo ya usafi wa mji.
4. Tatizo la kuwepo kwa upungufu wa sheria na kanuni ndogo ndogo za kiuendeshaji.

**Maoni na maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri Baraza kuanzisha mfumo wa uajiri kwa njia ya mkataba, hii itasaidia sana kuziba maeneo mambayo kuna upungufu wa wataalamu.
2. Vile vile Kamati inashauri kuwekwa mpango maalum katika utoaji wa elimu kwa wafanya biashara na kupewa uelewa juu ya lengo na azma ya Serikali katika ukusanyaji wa mapato.
3. Aidha, Kamati inaagiza Baraza la Mji Mkoani kujiwekea sheria na kanuni ndogo ndogo (by laws) katika kukabiliana na changamoto ndogo ndogo ndani ya Mamlaka yao.

**OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MJINI**

Kamati imeelezwa kuwa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini imeendelea na kufuatilia masuala mbali mbali ya kijamii ikikwemo afya, elimu, maji, ardhi na mazingira. Aidha, ofisi imefanya uhamasishaji wa vijana kujiunga na mabaraza ya vijana ambapo jumla ya vijana 95 wamehamasika kujiunga na mabaraza hayo.

vile vile ofisi imeimarisha vizuri suala la usalama kwa kufanya vikao mbali mbali kwa lengo la kujadili hali ya usalama katika Wilaya ya Mjini.

**Chnagamoto za Wilaya ya Mjini:**

1. Kamati imeelezwa kuwepo kwa ukosefu wa jengo la ofisi ya kudumu.
2. Kamati imeelezwa kuwa katika kutekeleza majukumu ya wilaya kisheria kesi zao hukwama Mahakamani kutokana na uendeshaji wa kesi wa DPP.
3. Kamati imehoji kuhusu uhalali wa Askari jamii kuchukua sheria mikononi mwao kwa kuwasumbua wananchi na wageni wanaoingia maeneo ya mjini pamoja na kufanya majukumu ya Askari Polisi.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inaagiza ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kutumia Kamati yake ya ulinzi na usalama kuhakikisha askari jamii wote kabla ya kupewa majukumu, wapewa elimu ya kutosha juu ya majukumu yao kwa raia na viongozi pamoja wageni wanaoingia ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Vile vile, Kamati inashauri Askari Jamii wa Mji Mkongwe ambao kwa kiasi kikubwa ndio wanaovunja sheria na kusababisha migogoro na wananchi wengi kukosa imani na Askari Jamii, ni vyema wakawekwa chini na kupewa elimu maalum ya maadili ya kazi.

2. Aidha, katika kuboresha utoaji wa msaada wa fedha za wazee; Kamati inashauri kuwekwa kwa Data Base System ambayo itahifadhi taarifa za wazee wa Wilaya mzima ya Mjini hivyo, kuepusha kujirudia kwa majina ya wazee waliokwisha sajiliwa.
3. Kamati imeshauri wazee ambao wamepewa pesa za wazee na hawastahiki kupewa na kutakiwa kuzirejesha fedha hizo, ni vyema wakaachiwa na adhabu hiyo ya kurejesha fedha wakapewa waliohusika kuwasijili wazee hao bila ya kuzingatia sifa.
4. Kamati pia, inashauri uongozi wa afisi kusimamia vyema vitendo vya uhalifu vinavyojitokeza siku hadi siku katika kulinda amani kwa wananchi na mali zao.

**WILAYA YA MAGHARIBI "A"**

Katika kipindi hiki cha Bajeti, Kamati imeelezwa kuwa ofisi imeratibu shughuli mbali mbali za miradi ya maendeleo na kusimamia utawala katika Wilaya hii.

**Changamoto zilizomo ndani ya Wilaya ya Magharibi "A":-**

i. Kamati imeelezwa kuwepo kwa vitendo vingi vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.
ii. Kamati imeelezwa kuwepo kwa migogoro ya Ardhi katika maeneo tofauti ndani ya wilaya hii.
iii. Kamati imeelezwa kuwepo kwa tatizo la kufoji nyaraka za mashamba na watu kujimilikisha mashamba hayo kwa nyaraka hizo za uwongo.
iv. Tatizo la upatikanaji wa hatimiliki za ujenzi wa afisi za shehia.
v. Uhaba wa wafanyakazi katika utawala na uendeshaji,
vi. Ubovu wa majengo, uhaba wa vyumba vya ofisi,
vii. Ukosefu wa vitendea kazi.

**Maoni na maagizo ya Kamati:**

1. Kamati imeshauri ofisi ya Wilaya ya Magharibi "A" kuwaita Masheha na kuwataka wafanye uchunguzi dhidi ya watoto wenye ulemavu ambao hawapati mahitaji yao ya msingi katika familia zao kama vile elimu na matibabu ili kuweza kuwasaidia kwa mujibu wa uwezo uliopo.
2. Kamati imeagiza ofisi ya Wilaya kuhakikisha kuwa imewafichuwa wote wenye kuendeleza vitendo vya ukatili na udhalilishaji na kuwapeleka katika vyombo vya Sheria bila ya kujali kupatiwa suluhu ya kifamilia.
3. Kamati inashauri uongozi wa Wilaya kuwahamasisha Masheha wao kutojiingiza katika migogoro ya Ardhi na ikitokea kesi hizo katika ofisi zao basi ni vyema kuelekeza katika taasisi zinazohusika na utatuzi wa migogoro ya Ardhi.
4. Aidha, Kamati inaagiza uongozi wa Wilaya kuhakikisha wamesimamia vya kutosha suala la upatikanaji wa Hatimiliki za maeneo wanayo miliki pamoja na majengo ya ofisi wanayotumia.

**AFISI YA MKUU WA WILAYA YA MAGHARIBI "B"**

Imeelezwa kuwa Wilaya ya Magharibi 'B' imefanya ufuatiliaji wa sekta mbali mbali zinazotekeleza shughuli zake ndani ya Wilaya ikiwemo kilimo, afya, elimu, mazingira, maji, mifugo na uvuvi pamoja na ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyovamiwa na kujengwa kinyume na taratibu. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwa ofisi imefanya utatuzi wa migogoro nane ya ardhi kati ya 14 iliyopokelewa.

**Changamoto za Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Magharibi 'B'**

1. Kamati imeelezwa kuwepo kwa ukosefu wa Majengo ya ofisi na hivyo kushindwa kwa watendaji kushiriki katika majukumu yao kikamilifu.
2. Kamati imeelezwa kuwepo ukosefu wa vyumba vya ofisi kumesababisha baadhi ya sekta kukosekana katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" kama vile Afisi ya Vitambulisho na Afisi ya Vizazi na Vifo.
3. Kamati imesikitishwa sana ni kuona katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuna kutengo cha madawa cha DHMT ambacho kimesababisha harufu kali na yenye kuharibu mandhari ya ofisi, hali hii inasababishwa na ufinyu wa ofisi na kulazimika kujibana katika jengo moja ambalo halikidhi mahitaji.
4. Kamati imeelezwa kuwepo kwa ufinyu na udogo wa ukomo wa bajeti ya ofisi hupelekea kushindwa kufanyika kwa majukumu ya msingi ya Wilaya kama vile ujenzi wa ofisi na kusaidia jamii pale inapofikwa na majanga ya kibinadamu.
5. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa matatizo ya migogoro ya ardhi katika sehemu mbali mbali ya Wilaya ya Magharibi 'B'.
6. Pila, Kamati imeleelezwa kuwepo kwa ongezeko la kesi za udhalilishaji wa kijinsia na ukatili kwa watoto.

**Maagizo na Maoni ya Kamati:**

1. Kamati inaagiza wizara ya Nchi OR Tawala za Mikoa Seriakli za Mitaa na Iadara Maalum za SMZ pamoja Wizara ya Afya kukaa pamoja na kulipatia ufumbuzi suala la uwekaji wa kitengo cha madawa cha DHMT kufanya utaratibu wa kukihamisha ndani ya ofisi ya Mkuu wa Wailaya na badala yake kitafutiwe sehemu inayostahiki.
2. Kamati pia, inashauri kuongezwa na kupatikana kwa wakati Bajeti ya ofisi ya Wilaya ya Magharibi 'B' ili kuweza kutatua mataizo mbali mbali yanayowakwaza ikiwemo uhaba wa ofisi.
3. Kamati inaagiza uongozi wa Wilaya kupitia Masheha wake kukwafichua wahalifu wote wanaojihusisha na kesi za udhalilishaji wa ukatili kwa watoto na watu wenye ulemavu, ili nao waweze kuishi kwa amani na utulivu katika jamii.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA – KITOGANI**

Halmashauri ya Wilaya ya kusini imefanya ufuatiliaji wa shughuli zake za kisekta zinazofanya kazi ndani ya Wilaya hii. Sekta zilizofanyiwa ukaguzi ni pamoja na kilimo, afya, elimu, uvuvi, misitu, mikugo, ardhi, mambo ya kale na ustawi wa jamii. Kamati imeelezwa kuwa katika Halmashauri hii imefanikiwa vizuri katika ukusanyaji wake wa mapato na hivyo imeshiriki katika umalizaji wa soko la wananchi Kitogani kwa kulitia sakafu na kuezeka.

**Changamoto za Halmashauri ya Kusini – Unguja:**

1. Kamati imeelezwa kuwa Halmashauri hii inakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi ambapo imelazimika kuajiri wafanyakazi wa muda – daily pay ambao wameajiriwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za Tume ya Utumishi. Aidha, Kamati imeelezwa mahitaji ya wafanyakazi wengine wawili kama vile afisa mtakwimu na afisa mipango.
2. Hatahivyo, Kamati imeelezwa kuwepo kwa tatizo la uhaba wa vitendea kazi na hivyo kukosa ubora wa shughuli zao za kila siku.

3. Vile vile, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya baadhi ya watu kukwepa kulipa kodi hasa wale wanaojishulisha na biashara za watalii.
4. Kamati pia imeelezwa kuwa hakuna takwimu halisi za ukusanyaji mapato katika madiko na masoko yote yaliyopo katika Halmashauri hii.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri uongozi wa Halmashauri kukaa pamoja na wamiliki wa jumuia zote zinazojihusisha na ukusanyaji wa kodi ili kujadili mustakbali mzima wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri.
2. Kamati inaagiza Halmashauri kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyake vya mapato bila ya kujali maslahi ya watu binafsi wanaokwepa kulipa kodi na kuinyima Serikali mapato yake.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI**

Kamati imeelezwa kuwa Halmashauri imejipanga vizuri katika kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi pamoja kuupokea mfumo wa *D by D* kwa kujitayarisha na ujenzi wa ofisi ili kuweza kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza kwa kuongeza wafanyakazi wenye uwezo kitaaluma, kuwajengea uwezo madiwani 12 na maafisa 8 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi ya sheria namba 7 ya Serikali za Mitaa na namba 8 ya Tawala za Mikoa, sheria zote ni za mwaka 2014.

**Changamoto za Halmashauri ya Kati:**

1. Kamati imeelezwa kuwa changamoto kubwa iliyopo ni kukosekana kwa kanuni madhaubuti ya Serikai za Mitaa ambayo ipo lakini bado haijawafikia katika ngazi za Halmashauri.
2. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa tatizo la kesi za udhalilishaji na ukatili katika maeneo mbali mbali ya Halmashauri.
3. Ukosefu wa usafiri, pia imeelezwa kuwa kikwazo katikakufanikisha majukumu ya Halmashauri hii.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri uongozi wa Halmasahuri kupatiwa elimu ili waweze kujitambua katika utekelezaji wa majukumu yao na ukusanyaji wa kodi na kutafuta vyanzo vipya vya mapato kama vile mahoteli, ujenzi wa nyumba za kuishi na madisko yanayopigwa katika mahoteli mbali mbali.
2. Kuhusu mfuko wa Jimbo, Kamati inashauri kutumika vizuri katika kuongeza na kusimamia miradi ya maendeleo ya wananchi kwa kushirikiana kati ya Halmashauri, Madiwani na Wabuge wenyewe.

**HALMASHAURI YA WIALAYA YA KASKAZINI ‘A’ UNGUJA**

Kamati imeelezwa kuwa katika Halmashauri hii kwa kushirikiana na ZANREC, imezindua kituo cha kusanifu na kuzirejesha taka katika matumizi mbadala. Vile vile imeotoa elimu kwa wafanyabiashara juu ya ulipaji kodi kwa hiari na ada za Halmashauri kwa wafanya biashara 750 waliomo katika Mamlaka ya Halmashauri. Aidha, Halmashauri imefanikiwa kutoa elimu ya kujingana na udhalilishaji wa wanawake na

watoto, athari za madawa ya kulevya pamoja na kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI.

**Changamoto za Halmashauri ya Kaskazini 'A'**

1. Kamati imeelezwa kuwepo kwa mvutano baina ya uongozi wa Halmashauri na ZMA kuhusu usajili wa vyombo vya baharini.
2. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa baadhi ya wananchi wanaokwepa kulipa kodi na hivyo kurudisha nyuma malengo yaliyokusudiwa.
3. Vile vile, Kamati imelezwa kuwa kumekuwepo kwa Ukakasi wa kutekeleza sheria no. 7 ya 2014 kuhusu Seriakli za Mitaa katika ngazi ya Halmashauri.
4. Kuhusu kesi za udhalilishaji na ubakaji bado limekuwa ni tatizo katika Halmashauri hii kutokana na jamii kulichukulia suala hili kama ni tatizo la familia inayoathirika.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inaagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' kukaa pamoja na Mamlaka ya usafiri wa vyombo vya Baharini kujadili kwa kutafuta njia muafaka wa mvutano wao kuhusu usajili wa vyombo vya Baharini kwa maeneo ya Halmashauri hii.
2. Kamati inashauri kuchukuliwa kwa hatua za lazima za kukomesha vitendo vya udhalilishaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto pamoja watu wenye ulemavu ili kujenga mazingira bora ya amani na usalama kwa wanajamii.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'B' UNGUJA**

1. Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeelezwa kuwepo kwa vyanzo vya mapato katika Halmashauri hii ambavyo vipo katika hatua ya mwisho kukamilika na kuanza kazi, vyanzo wenyewe ni machinjio ya ng'ombe ya Mahonda na Muwanda, pamoja na kiwanda cha matofali kilichopo Kipandoni katika kupanua ukusanyaji wa mapato yake.
2. Katika kukabiliana na tatizo la vitendea kazi, Halmashauri imefanya ununuzi wa gari moja la mzigo, gari moja la mkurugenzi na vespa nne ambazo zote zina fanya kazi.
3. Aidha, huduma za maji safi na salama zinapatikana vizuri katika matumizi ya kawaida ya wananchi pamoja na kupatikana kwa huduma za afya kwa mama mzazi na mtoto.
4. Hata hivyo, Kamati imeridhishwa sana na uamuzi wa Halmashauri kuanzisha uhusiano na Manispaa ya Morogoro Mjini kwa lengo la kujenga mashirikiano ya uekezaji kupitia miradi ya ujenzi wa machinjio ya ng'ombe na kilimo cha karafuu.

**Changamoto za Halmashauri ya Kaskazini 'B'**

1. Kamati imeelezwa kuwa changamoto kubwa ya Halmashauri hii ni kukosa Hatimiliki za majengo yake pamoja na viwanja wanavyomiliki.
2. Kamati meelezwa uwepo wa wafanyakazi wa mkataba – daily pay na wanapatiwa maslahi yao kwa mujibu wa sheria za utumishi zinavyoelekeza.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri watendaji wa Halmashauri wanaohusika na usimamizi wa afya kupita nyumba hadi nyumba katika kusimamia na kuhamasisha usafi katika suala zima la afya na kuhamasisha wazazi kupeleka watoto wao kupatiwa chanjo mbali mbali za kujinga na magonjwa hatari.

2. Pia, Kamati inashauri uongozi kusimamia vyema pamoja na kutoa hamasa kwa jamii kuacha masuala yote ya udhalilishaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto kutokana na wilaya hii kuongoza kwa vitendo hivyo.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI**

Pamoja na majukumu mengine ya kiutawala Halmashauri ya Micheweni imejipangia kutekeleza malengo yake kama vile kusimamia vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa mapato kupitia Halmashauri, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kuimarisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuimarisha huduma za usafi wa mazingira.

Aidha, Halmashauri pamoja na kugharamia shughuli za uendeshaji imeendelea na ujenzi wa ukumbi wa mikutano wa kisasa ikiwa ni sehemu ya uekezaji wake wa Halmashauri.

**Changamoto za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni:**

1. Kamati imeelezwa kuwa, kumepungua kwa vyanzo vya mapato vya Halmashauri ya Mimcheweni kwa kupelekwa Wilaya ya Wete na hivyo kusababisha kushuka kwa mapato na kuathiri malengo waliyojipangia.
2. Pia, Kamati imeelezwa uwepo wa changamoto ya kesi za udhalilishaji na ukatili katika Halmashauri hii ingawa ni kwa kiwango cha chini ukilinganisha na maeneo mengine ya Pemba.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri viongozi wa Halmashauri kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa hakuna mianya ya kupotea kwa mapato hayo.
2. Vile vile Kamati inashauri uongozi wa Halmashauri kusimamia kikamilifu hali ya amani iliyopo na kutowaachia watu wenye kuleta viashiria vya uvunjifu wa amani, sambasamba na hili, pia Kamati inaagiza Halmashauri kuwachukulia hatua kali wale wote wenye kuendeleza vitendo vya udhalilishaji na ukatili dhidi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

**C) IDARA MAALUM ZA SMZ**

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ilifanya ziara ya kutembelea vikosi vyote vitano (5) (KMKM, JKU, Mafunzo, KZU na KVZ) kwa upande wa Unguja na Pemba na kujionea shughuli zao mbali mbali za kizalendo na kuleta maendeleo ndani ya Nchi.

Aidha, Kamati inapongeza sana juhudi zinazofanywa na wapiganaji wetu wa vikosi hivi kwa kazi nguvu na nzito wanazozifanya za kulinda usalama na kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu katika Nchi yetu.

Samba samba na hayo, Kamati katika ziara yake hiyo imeweza kubaini changamoto mbali mbali zinazorudisha nyuma maendeleo ya Idara hizi kama ifuatavyo:-

1. Kuwepo kwa maslahi madogo ya wapiganaji wa vikosi vya SMZ;
2. Kuwepo kwa majengo na vitendea kazi ambavyo havikidhi haja ya askari wetu;
3. Kuwepo kwa ukosefu wa sare (uniform) za askari;
4. Kuwepo kwa ukosefu wa Hatimiliki na zaidi kwa upande wa vituo vya Pemba;
5. Tatizo la kutoshirikishwa kwa maafisa wa vikosi vya Pemba katika uandaaji wa Bajeti za Idara zao;
6. Tatizo la kutokuwa na sub-vote kwa upande wa Pemba.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inaishauri Serikali katika kupigania majengo na makaazi mazuri, uniform za askari wake pamoja na mambo mengine, basi isiwaachie vikosi peke yake katika kulishughulikia changamoto hizi.
2. Vile vile, Kamati inaagiza katika uandaaji wa Bajeti ya Idara Maalum, wakuu wote wa vikosi vilivyopo Pemba washirikishwe kikamilifu katika uandaaji wa Bajeti zao pamoja na wahasibu wao au maafisa watakao husika katika uandaaji wa Bajeti.
3. Kamati inaishauri Serikali iangalie suala la kuanzisha kiwanda ambacho kitashughulika na utengenezaji wa Sare na viatu vya askari wetu ili kuepusha gharama kubwa inayotumika kwa kuagizia nje ya Nchi.
4. Kamati pia, inashuri Serikali kuandaa bima ya afya kwa wafanyakazi wote wa Idara Maalum katika kuwajengea mazingira mazuri ya utendaji wao, aidha Kamati inaitaka Serikali kuanzisha mfuko wa Hifadhi ya jamii kwa upande wa vikosi vya SMZ kwa kuangalia utaratibu unaotumika wa vikosi vya ulinzi vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
5. Kamati inaagiza Wizara kufuatilia maeneo yote ya Kambi za Idara Maalum na kusimamia upatikanaji wa Hatimiliki za maeneo hayo hususan kwa upande wa Pemba.
6. Kwa vile Serikali imeamua kuanzisha tena utaratibu wa kuwapeleka vijana kujenga Taifa, Hivyo, Kamati inaishauri Serikali iwapatie vijana wa kutosha Jeshi la Kujenga Uchumi ili kuweza kuzalisha mali kwa kiwango kizuri.
7. Kamati inaona ipo haja ya kuwa na vituo vya Afya katika kambi zetu zote za Unguja na Pemba ambavyo pia, hutumiwa na Wananchi jirani wa Kambi hizo.

**KIKOSI MAALUM CHA KUKZUIA MAGENDO – KMKM**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kina jukumu la kuhakikisha kuwa kinazuia usafirishaji wa mali yoyote ambayo imezuiwa kisheria kusafirishwa baharini na nchi kavu kwa namna yoyote kutoka nje ya mipaka ya Zanzibar. Katika kuhakikisha kuwa majukumu yake yanatekelezeka, Kamati ya Sheria na Utawala Bora na Idara Maalum iliandaa ziara maalum ya kuvitembelea vikosi vyake mbali mbali Unguja na Pemba kwa lengo la kujionea baadhi ya majukumu yake pamoja na yanavyo kabiliwa na changamoto mbali mbali katika uendeshaji.

**Chnagamoto za Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo:**

1. Kamati imeelezwa kuwa tatizo kubwa la KMKM kamandi ya Pemba ni kukosa Hatimiliki za maeneo ya vituo vyake.
2. Kikosi cha KMKM kinauhaba wa mahanga ya askari na maafisa wake walio vituoni Unguja na Pemba.
3. Kamati ilifanya ziara yake katika kituo cha Makombeni na kuelezwa kuwa ndani ya kituo hicho kuna barabara ambayo wananchi wanapita na kuitumia kwa shughuli za kilimo na makaazi katika maeneo ya kituo.
4. Kamati pia, ilitembelea kambi ya Sengenya Mtambwe na kubaini kuwa Rada iliyopo haifanyi kazi kwa muda mrefu, aidha, katika ziara ya Msuka Kamati imeona uwepo wa muingiliano wa raia katika maeneo ya Kambi kwa shughuli za uvuvi.

**Maoni na Maagizo ya Kamati kwa KMKM:**

1. Kamati inashauri KMKM Pemba waboreshewe mawasiliano katika kukabiliana na wahujumu wa uchumi katika njia za baharini.
2. Kamati inaagiza Wizara kwa kushirikiana na Kamandi ya Pemba wasimamie maeneo yote ya vituo vilivyokuwa havina Hatimiliki na kuhakikisha zimepatikana, kwa kuishauri Seriakali kulipa fidia kwa wamiliki wa maeneo ambayo yamewekwa kambi ili kutoa fursa za kuendelea kwa shughuli za kiaskari.
3. Kamati inaishauri Serikali kununua Rada mpya kwa kituo KMKM Sengenya kwani iliyopo sasa haifai kwa matumizi ya ulinzi na usalama.

**JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)**

Jeshi la kujenga Uchumi ni miongoni mwa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo jukumu lake kubwa ni kutoa mafunzo kwa vijana katika Nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Vile vile kuwafunza vijana ufundi, kazi za amali na uzalendo ili kuwafanya vijana hao waweze kujitegemea na waweze kutumikia na kujenga nchi yao. Dhamira ya JKU ni kuchangia kuimarisha uchumi kwa kutoa mafunzo ya uzalishaji, ufundi na kazi za amali, mila, utamaduni na uzalendo.

**Chnagamoto za JKU**

1. Kamati imeelezwa kuwa Jeshi la JKU linakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha za matumizi mengineyo unaopelekea kupunguza kiwango cha ufanisi wa shughuli zao.
2. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa upungufu na uchakavu wa miundombinu ikiwemo mahanga kwa ajili ya maaskari wake.
3. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa tatizo la ukosefu wa Hatimiliki kwa baadhi ya maeneo ya vituo na mashamba ya Jeshi la JKU na kusababisha maaeneo hayo kuchukuliwa kwa shughuli za kiraia.
4. Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa watenda kazi na miundombinu ya maji katika mashamba yao hali inayosababisha upungufu wa uzalishaji.
5. Kamati pia imebaini utata wa matumizi ya eneo la shamba la Bonde Kwapweza katika ya ZAWA na JKU.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri katika kuimarisha shughuli za kilimo, kikosi cha JKU kiweke mikakati madhubuti ya kupata maji ili kujikita katika kilimo cha umwagiliaji badala ya kusubiri msimu wa mvua. Aidha, kwa yale mashamba yaliochoka ni vyema kupumzishwa ili kuyapa nafasi ya kujirudia au kubadilisha aina ya kilimo.
2. Kamati pia inalishauri Jeshi la Kujenga Uchumi kuwapatia zaidi askari wake utaalamu wa kilimo badala ya kutegemea askari wachache ambao muda wao wa kustaafu umekaribia.
3. Vile vile, Kamati imetembelea vituo mbali mbali na kuona makazi yake hayako katika hali ya kuridhisha, hivyo Kamati inashauri kuimarishwa kwa mahanga ya askari katika vituo mbali mbali ambavyo vinatumika na vinalinda usalama wa nchi yetu.

**CHUO CHA MAFUNZO ZANZIBAR**

Chuo cha Mafunzo ni miongoni mwa Idaraza Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ipo ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Idara ina jukmu kubwa la kuwapokea wale wote

wanaopelekwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa Sheria, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha tabia ili wanaporejea katika jamii wawe raia wema. Urekebishaji unajumuisha fani mbali mbali za kazi za mikono, ujenzi, ushoni, ufundi magari, ufundi kuchonga pamoja na huduma za ushauri nasaha.

**Changamoto za Chuo ca Mafunzo Zanzibar:**

Katika ziara iliyofanywa na Kamati katika vituo mbali mbali changamoto zifuatazo zilijitokeza:-

1. Kamati ilielezwa katika baadhi ya kambi katika Chuo cha Mafunzo kuwepo kwa tatizo la ukosefu wa Hatimiliki za maeneo ya Kambi pamoja na mashamba wanayoyatumia kwa ajili ya kilimo ikiwemo kambi ya Kengeja.
2. Kamati katika baadhi ya vituo ilielezwa kuwepo kwa ukosefu wa usafiri wa uhakika ikiwemo, Ubago, Kengeja na Kangagani.
3. Vile vile, Kamati katika ziara yake ilielezwa kuwepo kwa ukosefu wa huduma za afya katika kambi za Kengeja, Kangagani na Tungamaa.
4. Hata hivyo, Kamati imeona kuwepo kwa uchakavu wa majengo ya ofisi, ubovu wa nyumba za kuishi askari pamoja na uchakavu wa jela za wanafunzi. Hali hii imebainika katika vituo mbali mbali kama vile gereza la Kilimani, Tungamaa, Kangagani na Kengeja.
5. Aidha, Kamati imeelezwa kuwepo kwa ufinyu wa Bajeti na fedha za matumizi mengineyo katika idara ya Chuo cha Mafunzo pamoja na zone ya Pemba kutoshirikishwa kikamilifu katika uandaaji wa bajeti na hivyo kushindwa kuendesha miradi yake kutokana na uhaba wa fedha za matumizi.
6. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa tatizo la Kamanda mkuu wa Chuo cha Mafunzo Pemba kukosa uwezo na mamlaka ya kutoa ruhusa na likizo kwa maafisa wake walioko Pemba.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri wizara na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kuwa wanaweka mazingira mazuri kwa wapiganaji wake ili kuleta hamasa na ari ya ufanyaji kazi kwa askari wake. Hali hii inatokana na uhalisia ulioko Kisiwani Pemba kutokana na baadhi ya majengo ya ofisi kuwa chakavu na mbovu na hatari katika maisha ya binadamu. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa upatikanaji wa huduma ya uhakika ya maji safi na salama na madawa kwa askari na wanafunzi wake ni muhimu kupatikana.
2. Kamati inashauri Serikali inapoandaa bajeti kupewa vipaumbele mambo ya msingi katika Idara Maalum kama vile ujenzi na ukarabati wa ofisi pamoja na huduma nyengine za kibinadamu, vile vile askari wa Chuo wapatiwe chakula kama vikosi vyengine vya SMZ viavyopatiwa.
3. Kamati pia, ili elezwa kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali zinadaiwa na Idara ya Chuo cha Mafunzo, hivyo Kamati inaagiza madeni hayo yalipwe na Wizara isimamie kuhakikisha madeni yamelipwa kama mikataba yao inavyoelekeza.
4. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha wamesimamia Chuo cha Mafunzo katika kupata Hatimiliki za maeneo wanayoyatumia ili kuepusha kuchukuliwa na raia kwa shughuli zao mbali mbali.

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)**

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ chini ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa Idara Maalum za SMZ. Lengo la KZU ni kutoa huduma za kuzima moto na uokozi kwa ufamisi pamoja na kutoa elimu ya Zimamoto na uokozi kwa wananchi na Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi juu ya kinga na hadhari za moto.
Katika ziara iliyofanywa na Kamati katika vituo mbali mbali vya Unguja na Pemba, Kamati ilibahatika kuelezwa utekelezaji wa majukumu yao mbali mbali ambayo yamezidiwa na changamoto tofauti zinazoathiri utendaji wao.

**Changamoto za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU)**

1. Katika ziara iliyofanywa na Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika makao makuu ya KZU Kilimani imeelezwa kuwa wanakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa ukomo wa bajeti kulingana na mahitaji halisi ya kikosi hiki.
2. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa ukosefu wa vifaa vya kuzimia moto hususan katika vituo vya Zimamoto Bandarini na Uwanja wa Ndege Unguja na Pemba.
3. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa tatizo la ujenzi holela na usiokuwa na mipango ya nyumba za kuishi ambao hauendani na sheria za Zimamoto. Kikosi kinaomba katika kusimamia suala hili kishirikishwe wakati wa upangaji wa miji mipya inapoanzishwa katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.
4. Aidha, Kamati imeelezwa kutokuwepo kabisa kwa visima vya kuchukulia maji pamoja uchavu wa miundombinu ya maji (Fire Hydrant) kwenye maeneo mbali mbali ya mijini Unguja na Pemba.
5. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa sana na hali ya makaazi kwa baadhi ya vituo kwa Unguja na Pemba kwa kuona hakuna kabisa mahanga ya kuishi askari na hivyo hulazimika kujibana katika sehemu zao za ofisi jambo ambalo ni hatari kwa afya ya binadamu. Hali hii ilionekana katika vituo vya Mwanakwerekwe, Wete na Uwanja wa Ndege Kisiwani Pemba.
6. Kamati pia imesikitishwa ni kuona kituto cha KZU kilichopo Mkoani Pemba kinatumika kwa shughuli za parking ya Daladala jambo ambalo linaleta sura mbaya kwa jeshi hilo.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inaishuri Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga vituo vipya vya Zimamoto na Uokozi katika sehemu ambazo hazina vituo na vile vile kutoa kipaumbele kwa maeneo ambayo yameanzishwa na yaameshapatiwa Hati za ujenzi, maeneo hayo ni kama vile eneo la Kijichame Wilaya ya Micheweni Pemba.
2. Pia, Kamati inaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuwapatia askari wa kikosi hiki Bima ya Afya kutokana na kazi ngumu wanazozifanya za kuhatarisha maisha na afya zao kutokana na majanga ya moto.
3. Vile vile, Kamati inashauri kushirikishwa kwa vituo vyote vya KZU katika uandaaji wa bajeti hususan katika vituo vilivyopo Kisiwani Pemba ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazowakabili na kuepusha kumalizika kwa bajeti ya fedha za matumizi mengineyo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.
4. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya juhudi za makusudi ya kuwapatia kikosi vifaa vya Zimamoto pamoja na kuongeza ukomo wa Bajeti katika kutekeleza majukumu yake. Kutokana na ziara yake ya vituo tofauti, Kamati ilielezwa kuwepo kwa changamoto ya vifaa na hivyo kuwapa wakati mgumu katika utendaji wao.

**KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)**

Kikosi cha Valantia ni miongoni mwa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Jukumu la KVZ ni kuweka amani na utulivu katika nchi; kupambana na janga lolote litakaloikumba jamii; kulinda viongozi na mali za Serikali na kufanya kazi za kijeshi kwa lengo la kulinda hali inayohatarisha usalama wa Taifa. Katika ziara iliyofanywa na Kamati kupiti avituo mbali mbali vya KVZ iliweza kujionea maendeleo ya shughuli zao ambazo zimekwaza na changamoto mbali mbali kiutendaji.

**Changamoto za KVZ:**

1. Kamati imeelezwa kuwa, Kikosi kinakabiliwa na ufinyu wa ukomo wa bajeti usiokidhi mahitaji na kushindwa kuktekeleza mipango yake kama inavyojipangia.
2. Kamati pia, imebaini kuwepo kwa ukosefu wa mahanga ya askari na maafisa wao katika vituo mbali mbali kama vile Kambi ya Ndugukitu na Pujini Kisiwani Pemba.
3. Vile vile Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la ubovu wa barabara zinazoingia Kambini kwa vituo takribani vyote vya KVZ Kisiwani Pemba, kwa mfano Kambi ya Ndugukitu kwa Pemba ndio Makao makuu lakini barabara yake haikidhi mahitaji na inaleta usumbufu mkubwa wakati wa mvua.
4. Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa tatizo la usafiri na uchakavu wa magari katika kikosi cha KVZ hususan kwa upande wa Pemba hulazimika kutumia magari mabovu na yasiyokidhi haja au kuazima kutoka vikosi vyengine kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao.
5. Vile vile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa tatizo la kutoshirikishwa katika uandaaji wa bajeti kwa zoni ya Pemba na hivyo kutojua kiwango cha matumizi waliyopangiwa na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Maoni na Maagizo ya Kamati:**

1. Kamati inashauri wakati wa uandaaji wa bajeti kushirikishwa kikamilifu kwa KVZ Pemba, kwa kuwa mfumo wa bajeti tunaotumia ni wa PBB unatoa matumizi kwa mujibu wa utekelezaji wa shughuli ya Idara husika, basi ni vyema wakashirikishwa nao katika ngazi zote za maandalizi ili wapate kutoa changamoto zao zinazowakabili badala ya kufikiriwa tu matatizo yao.
2. Kamati inashauri katika kukiboresha kikosi hiki, ni vyema kupatiwa wataalamu wa fani mbali mbali ikiwemo wakandarasi, maafisa wa habari na maafisa Tehama.
3. Vile vile, Kamati inashauri kupatiwa bajeti yao kama walivyoomba na kuingiziwa kwa wakati ili kuweza kusaidia kutatua matatizo yao yanayowakabili. Sambamba ni hili Kamati inaagiza makao makuu ya KVZ, kushirikishwa moja kwa moja kwa zoni ya Pemba katika uandaaji wa bajeti ili kuweza kutoa changamoto zao wenyewe ambazo wamezipa kipaumbele katika kuzitatua na kuleta ufanisi katika majukumu yao.
4. Kamati inaishauri Serikali kuboresha miundo mbinu ya barabara zinazoenda Kambini katika vituo vyote ambavyo viko hali mbaya katika sekta ya barabara na usafiri.

## MAONI NA MAAGIZO YA JUMLA KWA WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

a) Kamati inaagiza Serikali za Mitaa kuwapa elimu watendaji wake wakiwemo masheha, madiwani na wafanyakazi wa kawaida ili kulingana na mabadiliko ya sheria na mazingira halisi ya utekelezaji wa sheria hizo.

b) Kamati inaagiza Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa wamefikia malengo waliyojipangia na wamesimamia vyema ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyao mbali mbali na kuhakikisha hakuna mianya ya uvujaji wa mapato hayo.

c) Vile vile, Kamati inashauri Serikali za Mitaa kusimamia vyema utoaji wa huduma za kijamii na kuhakikisha kila mmoja zimemfikia na kwa kiwango chenye ubora.

d) Kamati inashuri kwa Manispaa na Mabaraza ya Miji kuhakikisha wameajiri wataalamu mbali mbali katika kuleta ufanisi wa majukumu yao.

e) Kamati pia, inashuri Serikali kuandaa bima ya afya kwa wafanyakazi wote wa Idara Maalum katika kuwajengea mazingira mazuri ya utendaji wao.

f) Kamati inaishauri Wizara kufuatilia maeneo yote ya Kambi za Idara Maalum na kusimamia upatikanaji wa Hatimiliki za maeneo ambayo hayana Hatimiliki kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

g) Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya Masheha ambao uwezo wao wa kazi umepunguwa kutokana na ugonjwa au umri mkubwa, hivyo Kmati inaagiza wizara kufanya mabadiliko ya Masheha ambao uwezo wao wa kazi umepungua kutokana na ugonjwa, umri mkubwa au kukosa uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

**<u>HITIMISHO</u>**

Katika kutimiza wajibu na majukumu yake Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, imeitumia vyema Kanuni ya 106 (1) ya mwaka 2016 na kutoa ushauri na maelekezo ambayo matumaini yetu ni kuleta ufanisi katika ukamilishaji wa majukumu ya kila siku kwa Serikali, kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa pamoja na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maaalumu za SMZ.

Aidha, Kamati inashauri kwamba wakati Kamati inapofanya ziara zake za kikazi basi awepo Katibu Mkuu au Waziri wa Wizara husika ili kujua matatizo yanayokabili Taasisi za Idara zao.

Hivyo, maelekezo na maoni haya yametolewa na Kamati kwa lengo la kuleta ufanisi ndani ya Idara na Taasisi za Wizara husika katika kutafuta mustakbali mzuri wa maendeleo endelevu ya jamii ya Wazanzibari.

Kamati inawashukuru sana Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar pamoja na watendaji wengine wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi waliochangia kwa njia moja ama nyengine katika kufanikisha majukumu ya utekelezaji wa kazi za Kamati hii.